**TRA** yatekeleza agizo la Majaliwa

UKURASA 4



**WENYE** bucha za nyamapori walia masharti magumu

UKURASA 3



Uongozi na wafanyakazi wa gazeti la Nipashe unawatakia Watanzania wote sikukuu njema ya Eid- El- Fitr.

**Mhariri**


# Nipashe

Ijumaa Mei 14, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580580

www.ippmedia.com

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710


# UPANDIKIZAJI MIMBA

## **KILA** siku wanawake wanne watinga Muhimbili...*Endelea Ukurasa 2*



Waumini wa dini ya Kiislamu wa madhehebu ya Sunni, wakiswali swala ya Eid El Fitri, katika eneo la wazi, Kitunda Kati, jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Ajira zingine mamia zamwagwa serikalini

UKURASA 2

# MWINYI ASAKWA NA POLISI UINGEREZA

UKURASA 4

**MICHEZO** **YANGA YAIPIGIA HESABU NAMUNGO** UK. 24

**MAONI, KATUNI UK. 6**

# Upandikizaji mimba kuanza

**Na Mary Geofrey**

TATIZO la wanawake kushindwa kupata ujauzito, limeongezeka kwa kasi nchini huku wastani wa wanawake wanne huripoti katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH), kila siku kuwa na tatizo hilo.

MNH ipo mbioni kuanza kutoa huduma ya upandikizaji wa mimba, ambayo kitaalamu inajulikana kama In Vitro Fertilization (IVF), kabla ya kumalizika kwa mwaka huu (2021).

Nchi nyingine kwa Afrika Mashariki inayotoa huduma hiyo ni Kenya.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu jana, jijini Dar es Salaam, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano kwa Umma wa MNH, Aminiel Aligaesha, alisema baada ya kukamilisha maandalizi yote muhimu wataanza kutoa huduma hiyo. "Kazi inayoendelea kwa sasa ni ya matayarisho ya kuanza kutoa huduma ambayo ni ujenzi wa miundombinu na ununuzi vifaa vya matibabu," alisema Aligaesha.

Alifafanua kuwa, madaktari na wataalamu wa kutoa huduma hiyo wameshaandaliwa na tayari wako mafunzoni kwa ajili ya kujinoa kitaalamu.

Alisema huduma hiyo wataanza kuitoa kwa kushirikiana na wataalamu wa nje na ndani waliopata mafunzo ya utaalamu huo.

"Kama ilivyo kawaida yetu kwa huduma mpya tunazoanzisha hapa Muhimbili, huwa tunashirikiana na wataalamu kutoka nje ya nchi ambao wamebobea na baada ya kufanikisha na kuwajengea uwezo wataalamu wetu wa ndani huwa tunaendelea kutoa huduma wenyewe, " alisema Aligaesha.

Mapema wiki hii, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Doroth Gwajima, akiwasilisha bajeti kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa mwaka 2021/22 bungeni, jijini Dodoma, alisema katika kipindi cha mwaka 2021/22, Muhimbili itatekeleza mambo makuu manne ikiwamo kupandikiza mimba.

Alitaja huduma nyingine kuwa ni kupandikiza uloto (bone marrow transplant) kwa wagonjwa wenye kansa ya damu na kuendelea na ujenzi wa jengo la wagonjwa binafsi (private wards) lenye vitanda 200.

"Tutaendeleza huduma zote za kibingwa kama vile upasuaji kwa kutumia tundu dogo, upasuaji wa kichwa, shingo na koo," alisema Waziri Gwajima.

**UPANDIKIZAJI MIMBA NI NINI**

Katika hali ya kawaida, mimba hutunga kupitia tendo la ndoa pale mbegu za kiume ama manii zinapoungana na yai la mwanamke.

IVF ni mchakato wa kuunganisha yai la mwanamke na mbegu za mwanaume nje ya mwili wa binadamu katika maabara na kisha kurudishwa kwenye mwili wa mwanamke ili mimba ikue. Utaalamu huo uligunduliwa na wanasayansi watatu wabobezi wa magonjwa ya uzazi kutoka nchini Uingereza ambao walikuwa wanatafuta njia mbadala kwa wanawake wanaoshindwa kushika mimba kwa hali ya kawaida.

Wanasayansi hao ni Profesa Robert Edwards, Dk. Patrick Steptoe na Dk. Jean Purdy.

Kwa mujibu wa jarida la Science Daily, kufikia Julai 2018, takriban watoto milioni nane walizaliwa kwa kutumia utaalamu huo duniani.

**HATUA ZA UPANDIKIZAJI**

Idara ya Huduma za Afya ya Uingereza (NHS) imeorodhesha hatua sita zinazofuatwa na madaktari wa upandikizwaji wa mimba.

Hatua ya kwanza ni kusimamisha mzunguko wa kawaida wa hedhi.

Hatua ya pili ni kuboresha uzalishaji wa mayai. Mwanamke hupatiwa homoni ya FSH (inaongeza idadi ya mayai ambayo ovary; mfuko ambao mayai huzalishwa kwenye mwili wa mwanamke). Homoni hiyo hutolewa kwa njia ya sindano kwa siku 10 mpaka 12 mfululizo.

Hatua ya tatu ni kukagua maendeleo ya hatua mbili za awali. Vipimo mbalimbali hufanywa ikiwamo kupiga picha (ultrasound) ya ovari. Saa 34 mpaka 38 kabla ya mayai kuvunwa, mwanamke anayepitia matibabu haya huchomwa sindano ya mwisho ya homoni ambayo inasaidia mayai kukomaa.

Hatua ya nne ni kuvuna mayai kutoka kwenye mwili wa mwanamke. Yatavunwa kotoka kwenye ovari kwa kutumia sindano maalumu inayopitishwa kwenye uke. Hatua hii huchukua dakika 15 mpaka 20 kukamilika. Baadhi ya wanawake hupata maumivu kidogo ya tumbo.

Hatua moja anayopitia mwanaume nayo hufanyika, ambapo hutakiwa kutoa manii na kuiwasilisha hospitali haraka iwezekanavyo na wataalamu watachukua mbegu bora zaidi kwa ajili ya kuzitumia kwenye hatua ya tano ya mwanamke. Hatua ya tano ni kurutubisha yai. Hii inafanyika kwenye maabara, wataalamu wanaunganisha yai na mbegu za mwanaume na yai la mwanamke.

Baada ya saa 16 mpaka 20 madaktari huangalia kama yai limerutubishwa vyema.

Hatua ya mwisho ni kuhamisha kiini tete kutoka maabara mpaka mji wa mimba.

Si mara zote IVF hufanikiwa, na inapotokea hali kama hiyo, madaktari hutoa ushauri wa kitabibu na kupewa fursa ya kuamua kujaribu tena.

## Bosi MSD huru kesi ya uhujumu uchumi

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam imemwachia huru Mkurugenzi wa zamani wa Bohari ya Dawa (MSD), Laurean Bwanakunu, pamoja na Mkurugenzi wa Lojistiki, Byekwaso Tabura, baada ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kuwasilisha hati ya kuwaondolea mashtaka.

Upande wa Jamhuri uliwasilisha maombi ya DPP mahakamani kwamba hana nia ya kuendelea kuwashtaki vigogo hao dhidi ya kesi ya uhujumu uchumi iliyokuwa inawakabili.

Mahakama hiyo iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Kassian Matembele, ilipokea maombi hayo mapema jana, ambapo Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, aliomba kuwasilisha hati hiyo iliyotiwa saini Mei 10, 2021 na aliyekuwa DPP (sasa Jaji mteule), Biswalo Mganga.

Hakimu alisema baada ya mahakama yake kupokea hati ya DPP haina pingamizi inawaachia huru washtakiwa kama Jamhuri ilivyoomba.

Katika kesi ya msingi, washtakiwa hao walikuwa wakikabiliwa na mashtaka matano ikiwamo utakatishaji wa Sh. bilioni 1.6.

Ilidaiwa kuwa kati ya Julai 1, 2016 na Juni 30, 2019 katika maeneo mbalimbali ya jiji na mkoa wa Dar es Salaam wakiwa watumishi wa umma kwa pamoja walitengeneza genge la uhalifu kwa ajili ya kujipatia faida.

Katika shtaka la pili ilidaiwa kuwa kati ya Julai 1, 2016 na Juni 20, 2019 washtakiwa wote kwa pamoja waliisababishia hasara MSD hasara ya Sh. bilioni 3.816.

Jamhuri ulidai kuwa Bwanakunu akiwa ni mtumishi wa umma alifanya matumizi mabaya ya madaraka kwa kuongeza mishahara na posho za wafanyakazi bila ruhusa ya Katibu Mkuu Utumishi na kuisababishia MSD hasara ya Sh. milioni 85.199.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mohamed Mchengerwa (kushoto), akitoa hatimiliki kwa mmoja wa wananchi wa Shehia ya Welezo, wakati wa ziara yake ya kikazi ya kukagua utekelezaji wa miradi ya MKURABITA, visiwani Zanzibar jana. **PICHA: JAMES MWANAMYOTO**

# Serikali yatangaza ajira zingine 500 kada za afya

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imetangaza maombi ya ajira zingine 547 za kada mbalimbali za afya na watumishi hao wapya watakuwa chini ya Wizara ya Afya na taasisi zake.

Akizungumza kuhusu ajira hizo jana, Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Prof. Abel Makubi, alisema wizara hiyo imepokea kibali cha ajira hizo kutoka Ofisi ya Rais - Utumishi ikiwa ni utekelezaji wa ahadi iliyotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan kuajiri watumishi wapya takriban 40,000.

" Alibainisha kuwa kati ya ajira hizo, 473 zitaratibiwa na wizara hiyo na nafasi 74 zitaratibiwa na Sekretarieti ya Ajira.

"Wataalamu hawa 74 wa kada mbalimbali wataajiriwa katika Maabara Kuu ya Taifa na wataalamu 473 wa kada mbalimbali wataajiriwa katika Hospitali za Kanda za KCMC, Mbeya, Bugando na Benjamin Mkapa, Hospitali za Rufani za Mikoa na vyuo vilivyopo chini ya Wizara ya Afya," alifafanua.

Alisema maabara hiyo ambayo iko mkoani Dar es Salaam, imekuwa na tatizo la uhaba wa watumishi wa kada hiyo kwa muda mrefu na serikali imeona suala hilo na kutoa kibali cha kuajiri wataalamu hao 74.

Alitaja kada zitakazonufaika na ajira 473 kuwa ni pamoja na madaktari, wauguzi, wafamasia, wateknolojia wa dawa, wateknolojia wa maabara, wateknolojia wa mionzi na wateknolojia wa macho.

Wengine ni watoa tiba kwa vitendo, maofisa afya mazingira, wasaidizi wa afya, makatibu afya, maofisa ustawi wa jamii na maofisa lishe.

"Ajira hizo (473) zitajaza nafasi zilizoachwa wazi na watumishi waliokoma utumishi kutokana na sababu mbalimbali. Waombaji wanasisitizwa kuzingatia maelekezo yote yatakayotolewa na vyanzo rasmi vya taarifa za ajira, wataomba kwa kutumia kiunganishi ajira.moh.go.tz kuanzia tarehe 12-25, Mei mwaka huu," alisema.

## HABARI KITAIFA

# Wamiliki wa bucha za wanyamapori walia

**Na Romana Mallya**

MDAU wa bucha za wanyamapori mkoa wa Dar es Salaam, Shafii Mohamed, ameiomba serikali kuwaongezea wanyama wa kuwinda ili kuwaondolea mzigo mkubwa wa gharama za uwindaji, usafirishaji na uuzaji wa kitoweo hicho.

Akizungumza na Nipashe jana katika moja ya bucha linalouza nyamapori mkoani humo, Mohamed alisema gharama za uwindaji ni kubwa hivyo wamelazimika kuzifidia kwenye uuzaji wake ili kuepuka hasara.

Alitolea mfano uwindaji wa nyati ni Sh. 100,000 ambapo hawaruhusiwi kuondoka porini na zaidi ya mmoja hivyo wamekuwa wakimuuza kilo moja Sh. 14,000 ili kufidia gharama zote wanazotumia.

Alisema nyati wanamuuza kwa bei hiyo kwa sababu ni mkubwa lakini wanyama wengine bei ya kilo moja ni Sh.15,000.

"Wanyama wote tunaowauza hatuuzi zaidi ya kilo tatu hii ni kwa sababu ya changamoto ya upatikanaji wake na uhitaji kwenye soko ni mkubwa hivyo tunataka kila mtu aweze kupata, tukiuza kilo nyingi maana yake watu wengi watakosa," alisema.

Alisema biashara hiyo aliianza Machi 14, mwaka huu, ambapo wanauza nyati, pofu, kongoni, swala na sungura.

Alisema watu wengi wamekuwa wakipenda nyama ya swala, pofu na kongoni.

Alisema serikali imewapangia sehemu kama nane za kuwinda ambazo ni Kilwa, Simanjiro, Manyoni, Tabora, Katavi, Ifakara na Kisarawe ambapo baadhi kuna matatizo hakuna wanyama wengi.

Alisema wanapokwenda Kilwa gharama zake siyo chini ya milioni 3.5 ambapo ndani yake kuna fundi wa gari, wapishi, wawindaji wawili, ununuzi wa risasi ambazo kwa sasa zimepanda bei.

Alisema bei ya risasi ya kumuua mnyama mkubwa ni Sh. 35,000 hadi 40,000 na wadogo ni Sh. 13,500.

Alisema matatizo mengine ni kwa mkuu wa wanyamapori ambapo kila mnyama hawaruhusiwi kuchukua zaidi ya mmoja.

"Unapewa kibali cha kupiga nyati na labda unakuta unataka wawili lakini hauruhusiwi, utapewa kila aina ya mnyama mmoja mmoja, ambapo unakuwa na wanyama wanne au watano, ukipiga hesabu hupati kilo 600 utaambulia kilo 500 kwa sababu utumbo huwa tunawaachia wanakijiji ili usiharibike njiani," alisema.

Mohamed alitaja matatizo mengine ni kibali wanachopewa wakati mwingine kinaisha na wanyama waliowalipia wanapofika porini wanawakosa hivyo kwao ni hasara.

Alisema wiki mbili zilizopita kila mnyama amepanda mara mbili hivyo kwa sasa nyati badala ya kuwa Sh. 100,000 ni Sh. 200,000 na watakuwa wanapewa wawili.

Alisema wateja wao ni mchanganyiko lakini hawawezi kuwauzia wa hoteli kwa sababu wanataka kilo nyingi na wao hawauzi zaidi ya kilo tatu.

"Endapo serikali ikiongeza idadi ya wanyama kwa kila aina maana yake ni kwamba bei ya kilo itapungua na wao wataweza kuuza zaidi ya kilo watatu kwa wateja wao. Tunataka kila mtu anunue," alisema.

Alisema mzigo unapoingia Dar es Salaam wanaweza kukaa nao hadi wiki moja na ili wapate kibali kingine cha uwindaji ni mpaka nafasi za wawindaji wengine ziishe hivyo huchukua hata miezi minne.

Alisema ndiyo maana waliomba waongezewe vitalu vya uwindaji ili nyama inapoisha buchani waende kuwinda tena badala ya kukaa kwenye foleni.

Alisema katika mwezi wa mfungo kwa siku walikuwa wanauza kilo 18 hadi 40 na wakati mwingine huuza hadi kilo 80.

# Kamati kushauri upatikanaji fedha za sekta kilimo rasmi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imeunda kamati maalum ya watu 10 itakayotoa mapendekezo ya namna ya kutafuta fedha za kusaidia sekta ya kilimo.

Kamati hiyo itafanya kazi kwa muda wa miezi minne na kubainisha namna fedha hizo zitakavyopatikana, itaongozwa na Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe. Akizungumza jana na waandishi wa habari, Prof. Adolf Mkenda alitaja wajumbe wengine katika kamati hiyo kuwa ni Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB, Ruth Zaipuna, Japhet Justine (Benki ya Kilimo), Theobat Sabi (NBC).

Wengine ni Sabasaba Moshingi Mtendaji Mkuu wa (TPB), Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Pass Trust, Ana Sanalingigwa, Charles Itembe (Azania Benki), Charles Ngili, Mtendaji Mkuu wa TIBFI, Benson Ndiege Mrajisi wa Vyama vya Ushirika.

Alisema Mrajisi amewekwa kwenye kamati hiyo kwa sababu suala la ushirika na kilimo vinaendana na Naibu Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Prof. Siza Tumbo ataisaidia kamati hiyo.

"Itafanya kazi ndani ya miezi minne kuchambua na kupokea maoni kutoka sehemu mbalimbali, itakuja na mapendekezo ya kutatua changamoto ya fedha na nyingine ambazo zipo katika kilimo," alisema Waziri Mkenda.

Aliitaka kamati hiyo iwasaidie katika suala la uzalishaji wa mazao ya mafuta kwa haraka, pamoja na sekta ya mazao mengine. "Tunataka kutengeneza mfumo ambao utasaidia benki kuwezeshe kwenye viwanda vya mafuta, watoe mikataba ya uzalishaji kwa wakulima wakubwa na AMCOS ikiwamo kuwasaidia kupata mbegu za kutosha," alisema Waziri Mkenda.

Kadhalika, alisema kuna balozi mbalimbali hapa nchini ambazo zina fursa ya fedha kwa kilimo na kuitaka kamati kuchambua fursa hizo ili kuona namna ya kuzipeleka maeneo ambayo yanauhitaji wa fedha hizo.

Prof. Mkenda alisema kumekuwa na tatizo la fedha hususani za mikopo kwa ajili ya kuendesha shughuli za kilimo. "Takwimu zinaonyesha kwamba fedha zinazotoka katika benki kwenda kwenye kilimo zinaonekana chache ambazo ni asilimia 9.2, wakati sekta ya kilimo inaajiri takribani asilimia 60 ya Watanzania," alisema.

Aliongeza: "Timu hii itasaidia kwa kiasi kikubwa kuhakikisha tatizo la fedha katika kilimo linakwisha, tunachangamoto pia katika bodi za mazao na vyama vya ushirika, hivyo kamati hii naamini itafanya vizuri kuhakikisha tunatatua suala la upatikanaji wa fedha katika sekta ya kilimo."






**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**

**(COMMERCIAL DIVISION)**

**AT DAR ES SALAAM**

**COMMERCIAL CASE NO. 128 OF 2020**

**SAO HILL INDUSTRIES LIMITED………………..……………………….PLAINTIFF**

**VERSUS**

**URBAN AND RURAL ENGINEERING SERVICES LIMITED……...............DEFENDANT**

**DECREE**

**WHEREFORE,** the Plaintiff prays for judgment and decree against the defendant as follows;

i. A declaration that the Defendant has breached the terms of the Purchase Agreement executed between the Parties.
ii. An Order for payment of **TZS 1, 823,564,330.00** being the outstanding amount due and owing to the Plaintiff for the purchase of the Poles supplied by the Plaintiff to the Defendant.
iii. An order for reimbursement of the CESS amount paid by the Plaintiff on behalf of the Defendant to the tune of **TZS 62,994,500.00.**
iv. An order for payment of **TZS 68,418,520.10** being the accrued interest on the outstanding payments for the supplied poles and CESS by the Defendant as at 7th September 2020.
v. An order for payment of an interest at commercial rate of 21% per annum on the Principal amount from the date of default until the date of Judgment.
vi. An order that the Defendant pay general damages to be assessed by the Court for breach of contract.
vii. An order that the Defendant to pay interest on the Decretal amount at Court rate of 12% per annum from the date of Judgment to the date of full satisfaction.
viii. Costs of this suit.
ix. An order for payment of interest on the costs at Court's rate of 12% from the date of Judgment until payment in full.
x. Any other order and relief as this Honourable court may deem fit and just to grant.

This matter is coming for judgment on this 4th day of May 2021 before Hon. B.K. Phillip, J in the presence of advocate Jovison Kagirwa for the Plaintiff and in the absence of the Defendant.

**THIS COURT DOTH HEREBY ORDER THAT**

i. The Defendant has breached the terms of the Purchase Agreement executed between the Parties.
ii. The defendant shall pay the plaintiff a sum of TZS. 977,407,430.00 being the outstanding amount due for the purchase of the Poles supplied to the defendant by the Plaintiff.
iii. The defendant shall pay the Plaintiff a sum of **TZS 62,994,500.00.** being the amount of CESS paid by the plaintiff on behalf of the Defendant.
iv. The plaintiff shall pay the plaintiff interest on the principal amount in item (ii) and (iii) herein above at commercial rate of 21% per annum from August 2020 the date of Judgment.
v. The Defendant shall pay the plaintiff interest on the decretal amount at Court rate of 7% per annum from the date of Judgment to the date of full payment of decretal sum.
vi. Costs of this suit shall be borne by the defendant

Given under my hand and seal of the court on this 4th day of May 2021.

THE HIGH COURT OF TANZANIA COMMERCIAL DIVISION

**B.K. PHILLIP**

**JUDGE**

Extracted on this 12th day of May 2021

# Mwinyi alivyosakwa na polisi Uingereza

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS mstaafu wa awamu pili, Ali Hassan Mwinyi, amesimulia alivyosakwa na askari polisi wa Uingereza baada ya kupoteza fedha alizokuwa nazo huko.

Katika kitabu chake cha 'Mzee Rukhsa, Safari ya Maisha Yangu', Mwinyi anasema tukio lilitokea mwaka wa masomo 1961/62 alipopelekwa na serikali kuchukua kozi fupi ya mbinu za ufundishaji wakufunzi wa vyuo vya ualimu katika Chuo Kikuu cha Hull kilichoko Leicester, Uingereza.

Anasema alikaa chuoni huko kwa muda mfupi kabla ya kutafutiwa chumba cha kupanga kwenye nyumba ya mjane, ambaye mumewe alifariki dunia kwa ajali ya gari.

"Ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa nafasi aliyonipa kuwapo ndani ya familia hiyo na kuwafariji.

"Kabla ya kumalizika ile wiki ya kwanza, niliona ile huzuni inayeyuka polepole na uchangamfu unachanua na kujipenyeza katika familia. Mwishowe, nyumba ilichangamka na furaha kuzagaa.

"Siku moja nilifikwa na jambo lililonitisha sana. Ilikuwa siku ya Jumatatu, baada ya kuoga na kupata kifungua kinywa, nikajitayarisha kutoka. Hapo ndipo nilipogundua kuwa sina pesa wala mkoba wake (mjane) ambamo mlikuwa ninaziweka!

"Hamadi nimeibiwa! Nikidhani. Nikatulia kwa muda kitandani nilipoketi nikifiri la kufanya," Mwinyi anasimulia.

Anaendelea na simulizi ya tukio hilo akisema aliamua kumshirikisha mwenyeji wake, Mama Jonathan kwamba "nimeibiwa fedha zangu zote na mkoba wake!"

"Mama Jonathan akaniambia: 'Tulia, kaa kitako. Nchi hii haina wezi. Wezi wanaokuwapo, tena kwa nadra, ni waliopo katika sinema, wanaovunja benki lakini hakuna wadokozi wala wakwapuzi.

"Hebu fikiri zaidi. Juzi na jana, ulitoka humu nyumbani; na kama ulitoka ulikwenda wapi? Na je, wiki hii hujanunua kitu chochote?"

Mwinyi anasema kuwa hapo akakumbuka na kumjibu mjane huyo kwamba Ijumaa iliyopita alikwenda kwenye duka moja la mbali kidogo na nyumbani na kununua dawa ya meno, ndipo mwenyeji wake akamtaka kwenda kwenye duka hilo muda huo.

"Nikaenda. Nilipofika karibu, mfanyakazi wa dule lile akaniwahi na kuniambia kwa sauti kubwa: "You have come for your money?" yaani: "Umefuata pesa yako?" Nikamjibu, ndiyo huku nikisogea.

"Nilipofika akafungua kibweta, akatoa pochi yangu na mimi nikanyoosha mkono kuipokea, akakataa kunipa; akaniambia nisubiri kidogo. "Akaifungua yeye ile pochi, akanihesabia pesa zilizokuwamo ndani yake. Alipokwisha akaniuliza: "Je, ndizo pesa hizi, hazijapungua?" Nikamjibu kuwa zipo sawa, hazijapungua; ndipo aliponikabidhi.

"Akaniambia: 'baada ya wewe kuondoka hapa ndipo tukaiona hii pochi hapa mezani. Tukajua ni yako. Hivyo tulipiga simu polisi na kuwapa wasifu wako ili ukamatwe na kurudishwa hapa tukukabidhi pesa zako'.

"Nikawashukuru na kuwaaga. Mpaka leo ninatamani duniani pote wanadamu tungekuwa na uaminifu wa kiwango hicho! Yamebaki matamanio. Sina uhakika kama hata huko Leicester uaminifu bado upo wa kiwango hicho.



Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, akizungumza na waandishi wa habari, kuhusu mwenendo wa kampeni za CCM katika majimbo ya Buhigwe na Muhambwe, mkoani Kigoma jana, kuelekea uchaguzi wa marudio utakaofanyika kesho kutwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TRA yatekeleza agizo la Majaliwa siku hiyo hiyo

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Mapato (TRA) imesema ilianza juzi kutekeleza mara moja agizo la Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kwa kuondoa vikwazo kwenye Kituo cha Mizani cha Bandari ya Dar es Salaam.

Taarifa iliyotolewa jana, ilibainisha TRA mara moja ilimweka ofisa wake kuhudumia kituo hicho muda mfupi baada ya Waziri Mkuu kuondoka bandarini huko juzi.

"Kuanzia jana (juzi) tumetekeleza mara moja agizo la Waziri Mkuu kwa kuweka mtu wetu pale (Kituo cha Mizani bandarini)," alisema Mkurugenzi wa Huduma na Elimu kwa Mlipakodi wa TRA, Richard Kayombo.

Pia, alitaja hatua nyingine ambazo zote zinahusu forodha, ni za kuondoa vikwazo vya uondoshaji wa mizigo mipakani na maeneo mengine nchini, pia kuboresha ushirikiano na wadau wengine.

"Tunayo timu yetu ya ufundi ambayo inafanya kazi kwa saa 24 kwenye vituo vyote vya forodha. Wanahakikisha mifumo haileti shida na kunapokuwa na tatizo, basi watoe taarifa kwa wadau wote na kutoa njia mbadala," alisema.

Juzi, Majaliwa alifanya ziara bandarini Dar es Salaam, aliitaka Mamlaka ya Bandari (TPA) pamoja na TRA kurekebisha mifumo yao ili kuharakisha upakuaji mizigo.

Akitoa ufafanuzi kuhusu utatuzi wa vikwazo katika uondoshaji wa mizigo mipakani na maeneo mengine ya forodha, Kayombo alisema TRA imechukua hatua kadhaa ikiwa ni pamoja na kukutana na wadau wake.

Mkurugenzi huyo anabainisha kuwa hivi karibuni, mamlaka hiyo kwa kushirikiana na wadau wanaohusika na uondoshaji wa shehena, iliitisha kikao cha majadiliano kilichokuwa na lengo la kujadili na kuboresha uondoshaji shehena mipakani na maeneo mengine ya forodha.

Alibainisha kuwa kikao hicho kilihusisha taasisi za serikali ambazo ni Shirika la Viwango (TBS), Mamlaka ya Bandari (TPA), Wakala wa Serikali Mtandao (eGA), Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC), Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) na Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA).

Kayombo alisema kikao hicho pia kiliwahusisha wadau wasio wa serikali, ambao ni pamoja na uongozi wa Chama cha Mawakala wa Forodha Tanzania (TAFFA) na baadhi ya wanachama wake.

"Kikao hicho kiliongozwa na Kamishna Mkuu wa TRA, Alphayo Kidata, ambaye alisema serikali ya awamu ya sita imeweka msukumo mkubwa katika ukusanyaji wa mapato kwa ufanisi ili kuondoa mianya ya ukwepaji kodi na kuboresha mazingira ya biashara nchini kwa kutumia mifumo ya kielektroniki.

"Kamishna alisem msukumo huo ndiyo uliosababisha kuanzishwa kwa Mfumo wa Pamoja na wa Kielektroniki wa Uondoshaji Shehena Mipakani na Maeneo ya Forodha (Tanzania Electronic Single Window System - TeSWS) ili kurahisisha uondoshaji shehena," Kayombo alisema.

Mkurugenzi huyo alisema Kidata alibainisha faida za mfumo huo kuwa ni kurahisisha na kuwezesha biashara, kuongeza ufanisi wa matumizi bora ya rasilimali, kuongeza uhiari wa biashara kwa waingizaji na waondoshaji wa mizigo, kuimarisha usalama, kuongeza uadilifu na kuweka uwazi katika utendaji kazi pamoja na kupunguza biashara haramu.

"Faida nyingine ni kupunguza kwa kiasi kikubwa gharama, muda wa uondoshaji mizigo bandarini na vituo vya mipakani, kupunguza changamoto za uondoshaji wa shehena kwenye vituo vya forodha, kuongeza ari ya kulipa kodi kwa hiari miongoni mwa wafanyabiashara na kurahisisha ufuatiliaji wa mizigo kwa wakati," alisema.

Kayombo alimnukuu kiongozi huyo wa TRA akisema mfumo huo wa kielektroniki unaruhusu wadau wote wa biashara na wasafirishaji kuwasilisha kadhia za forodha na taarifa zote zinazohusu mizigo inayoingia, inayotoka pamoja na ile inayopita nchini kwenda nchi jirani mara moja tu ambapo kila mdau ataziona na kuzifanyia kazi.

Janeth Mosha, Ofisa wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano wa TRA, alisema mfumo huo unatekelezwa kwa awamu tatu. Alisema awamu ya kwanza inatumika tayari na jumla ya kampuni 489 zinatumia mfumo huo na taasisi nne za serikali zimeshaunganishwa na mfumo. Taasisi hizo ni TBS, TMDA, GCLA na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania (TAEC).

"Kadri siku zinavyozidi kwenda ndivyo mafunzo hutolewa kwa wamiliki wa kampuni zinazojishughulisha na shughuli za uwakala wa forodha na tunatarajia kampuni zote zilizosajiliwa takribani 913 zitumie mfumo huu," Janeth alisema.

Alibainisha kuwa awamu ya pili iko kwenye majaribio ya kiufundi na baada ya majaribio hayo, yatafuata majaribio ya watumiaji wa mfumo husika.

"Baada ya majaribio yote mawili, tunatarajia kufanya utaratibu wa kutumia awamu zote mbili kwa pamoja," Janeth alisema na kubainisha kuwa awamu ya tatu, iko kwenye taratibu za ujenzi.

Makamu wa Rais wa TAFFA, Waheed Saudin, aliusifia mfumo huo na kuomba marekebisho yafanyike ili kuondoa vikwazo wanavyokumbana navyo wakati wanapotumia mfumo huo wa uondoshaji shehena.

"Mfumo ni mzuri sana lakini kuna baadhi ya changamoto tumezileta kwenu kwa maandishi na nyingine mmezisikia hapa kutoka kwa washiriki, tunaomba mzitafutie ufumbuzi," alisema.

Kayombo alibainisha kuwa kikao hicho kilikuwa na washiriki 381 na kutokana na michango chanya iliyojadiliwa, Kamishna Mkuu wa TRA (Kidata) aliagiza kikao kingine kama hicho kifanyike Juni 26, mwaka huu, ili kupata mrejesho wa kufanyiwa kazi kwa waliyojadiliwa.

HABARI KITAIFA

# Sababu maboresho Ocean Road, MOI kukwama hii

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

UJENZI wa majengo na ununuzi wa vifaa tiba vya kuboresha huduma za afya katika Taasisi za Saratani Ocean Road (ORC) na Mifupa Muhimbili (MOI), umekwama kutokana na ukosefu wa fedha zilizoidhinishwa na bunge.

Fedha hizo ni Sh. bilioni 4 za ORC na Sh. bilioni 5 za MOI ikiwamo Sh. bilioni 1.8 zilizokopwa kwenye Mfuko wa Bima ya Afya wa Taifa (NHIF), na kuna zilizoidhinishwa na Bunge mwaka 2019/20 hazikupelekwa.

Hayo yamo kwenye taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, iliyowasilishwa juzi bungeni na Mwenyekiti Stanslaus Nyongo, wakati wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Alisema kamati hiyo ilitembelea ORC kuangalia ujenzi wa jengo maalum la kusimika mashine maalum, maabara za kuchanganyia dawa za nyuklia na vyumba vya huduma, ununuzi na usimikaji wa mashine ya cyclotron na ununuzi na usimikaji wa mashine ya PET/CT Scan vya Sh. 16,783,405,000.00 ikiwa ni bajeti ya tangu mwaka 2016/17.

Alisema serikali ilitoa Sh. bilioni14.5 na ORC ilitoa Sh. bilioni moja kwenye mapato yake ya ndani, kiasi ambacho ni pungufu ya fedha zilizokubaliwa na kuwa na nakisi ya Sh.1,283,405,000.00.

Alisema nakisi hii ikijumlishwa na fedha kwa ajili ya waranti katika mwaka wa pili na gharama za malighafi na uendeshaji wa kuanzia kiwanda, jumla kuu ya nakisi katika mradi huu ni Sh. 2,719,005,000.00, ambacho kiliifanya ORC kuomba fedha katika bajeti ya mwaka wa fedha 2020/2021 na Bunge liliidhinisha, Sh. bilioni 4.

"Hadi kamati inatembelea mradi huu, fedha hizi zilikuwa hazijatoka. Mradi huu ni muhimu sana kwa Taifa letu kutokana na ukweli kwamba utaboresha huduma za saratani nchini ziwe katika kiwango cha kimataifa hasa katika uchunguzi, kwani mashine hii ndiyo mashine ya kisasa kabisa katika uchunguzi wa saratani duniani kote," alisema. Nyingine ni kuunguza rufani za nje na hivyo kuokoa fedha ambazo serikali hugharamia wagonjwa nje ya nchi hasa India, kuongeza mapato ya ORC na kuongeza wagonjwa wa nje ya nchi.

"Inakadiriwa kuwa mashine itaweza kuhudumia takriban wagonjwa 2,000 kwa mwaka kutoka nje ya nchi, ambapo kila kipimo cha PET/CT Scan ni Sh. 1,600,000, hivyo kuingiza mapato ya wastani wa Sh. bilioni 3.2 kwa mwaka kwa huduma ya PET/CT Scan kwa wagonjwa kutoka nje ya nchi," alifafanua.

Nyongo alisema pia watapata mapato yatakayotokana na takribani wagonjwa 1,000 walio NHIF na binafsi, na kuingiza Sh. bilioni 1.6 kwa mwaka.

"Kamati inaendelea kusisitiza serikali kuhakikisha kiasi hicho cha Shilingi bilioni 4 kinatolewa kwa taasisi hii muhimu kabla ya mwaka huu wa fedha haujaisha ili mradi huu uweze kukamilika kama ulivyopangwa ifikapo Oktoba, 2021," alisema.

Mwenyekiti huyo alisema mradi wa MOI awamu ya III unaohusisha ujenzi wa jengo na ununuzi wa vifaa tiba na ulianza katika mwaka wa fedha 2017/18 na serikali ilitoa kiasi cha Sh. bilioni 16.5, kwa ajli ya ununuzi wa mashine za kisasa. Aidha, alisea katika mwaka wa fedha 2020/2021, kiasi cha Sh. bilioni 5 kilitengwa kwa ajili ya uboreshaji wa huduma kati yake Sh. bilioni 1.8 kwa ajili ya kulipa deni la NHIF la ujenzi wa MOI phase III, na Sh. bilioni 3.2 za ununuzi wa vifaa tiba.

"Hadi kamati inatembelea mradi huu, fedha hizo zilikuwa hazijatolewa. Kamati ilielezwa kuwa mawasiliano yameshafanyika na kwamba serikali imejipanga kuhakikisha kuwa fedha hizo zinatolewa kabla mwaka wa fedha wa 2020/2021 haujaisha," alisema.

"Kamati ililezwa changamoto ambazo ni kikwazo katika utekelezaji wa majukumu ya MOI ni pamoja na bajeti finyu ikilinganishwa na mahitaji halisi ya ununuzi wa vifaa na gharama za uendeshaji, miundombinu duni isiyokidhi mahitaji kwani wagonjwa ni wengi na maslahi duni ya watumishi ambayo yanapunguza morali ya utendaji kazi," alibainisha.



Mafundi wakiendelea na kazi ya ujenzi wa mifereji ya maji ya mvua katika eneo la Magomeni, Manispaa ya Kinondoni, mkoani Dar es Salaam jana. PICHA: MIRAJI MSALA

# Serikali inavyopunguza vifo wajawazito, watoto

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

SERIKALI imesema vifo vinavyotokana na uzazi vimepungua hadi 556 kwa kila kizazi hai 100,000, kutokana na jitihada za afua zilizowezesha upungufu huo.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Doroth Gwajima, alisema kwa mujibu wa matokeo ya Utafiti wa Hali ya Afya na Watu (TDHS) yaliyotolewa mwaka 2015/2016 ilionyesha kuwa vifo vitokanavyo na uzazi ni 556 kwa kila vizazi hai 100,000.

Aidha, utafiti huo pia ulionyesha katika kipindi hicho vifo vya watoto chini ya miaka mitano vilipungua kutoka 81 kwa kila vizazi hai 1,000 mwaka 2010 hadi 67 kwa kila vizazi hai 1,000.

Dk. Gwajima, alisema hayo wakati akiwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka 2021/22.

Alisema mafanikio hayo yametokana na afua zinazotekelezwa katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, ambazo ni kusisitiza umuhimu wa wajawazito kuhudhuria kliniki ipasavyo, kujifungulia kwenye vituo vya kutolea huduma za afya, utekelezaji wa kampeni ya jiongeze tuwavushe salama na kufanya tathmini na uanzishaji wa vyumba maalum kwa ajili ya matibabu ya watoto wachanga wagonjwa.

Kwa mujibu wa waziri, utafiti wa TDHS unaotarajiwa kufanyika kuanzia mwezi Novemba 2021 utatoa matokeo yenye kupungua kwa vifo vitokanavyo na uzazi na watoto.

Alisema katika kuimarisha huduma za afya kwa mtoto mchanga na kupunguza vifo vya watoto hao nchini, wizara imejiwekea lengo la kufikia asilimia 80 ya hospitali 350 (zinazomilikiwa na serikali, taasisi za dini, mashirika na watu binafsi) kuwa na vyumba maalum kwa ajili ya matibabu ya watoto wachanga wagonjwa ifikapo mwaka 2025.

Alisema katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, jumla ya hospitali 61 zilifanyiwa tathmini na kuagizwa kuanzisha vyumba hivyo katika mikoa 12, ambazo zinapaswa kuhakikisha uwapo wa vifaa na watoa huduma wenye stadi na ujuzi wa kuhudumia watoto wachanga, njiti na watoto wagonjwa wanaohitaji huduma hiyo.

Alisema katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, takwimu zinaonyesha wajawazito waliojifungulia kwenye vituo vya kutolea huduma iliongezeka hadi kufikia asilimia 81 ikilinganishwa na asilimia 63 kwa takwimu za mwaka 2015/16.

Waziri Gwajima alisema idadi ya kinamama waliojifungua na kurudi kliniki siku mbili baada ya kujifungua iliongezeka na kufikia asilimia 62 ikilinganishwa na asilimia 34 kwa mwaka 2015/16.

Aidha, alisema wizara kwa kushirikiana na wadau wake inaendelea kufanya ufuatiliaji wa takwimu za vifo vitokanavyo na uzazi.

Waziri Gwajima alisema katika kuimarisha mifumo ya upatikanaji wa dawa muhimu za afya ya uzazi, taarifa zinaonyesha kuwa katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, dozi 4,330,607 za dawa ya kukinga na kuzuia upungufu wa damu kwa wajawazito zilinunuliwa na kusambazwa katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini.

Alisema dawa nyingine muhimu ambazo ziliendelea kupatikana katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021 ni pamoja na dozi 327,220 za sindano ya Magnesium Sulphate kwa ajili ya kukinga na kutibu kifafa cha mimba.

Pia sindano za Dexamethasone ambazo hupewa mama kumsaidia mtoto kupumua inapotokea mjamzito yuko kwenye hatari ya kujifungua mtoto njiti, ilipatikana kwa asilimia zaidi ya 90 ya mahitaji katika vitu vya kutolea huduma za afya nchini.



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Serikali ifanyie kazi upungufu wa dawa

**MJADALA** wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, umetawaliwa na kilio kikubwa cha ukosefu wa dawa kwa wananchi, jambo ambalo limeharakisha vifo vya wengi.

Aidha, ukosefu wa huduma bure za afya kwa wazee, wajawazito na watoto ni kilio kingine kilichozungumzwa na kila mbunge aliyechangia mjadala huo wa mwaka wa fedha 2021/22.

Watunga sheria hao walitaka hatua madhubuti kuhakikisha dawa zinapatikana kwa kuwa wananchi wanateseka na hata kwenye Bima ya Taifa ya Afya (NHIF) na Mfuko wa Afya ya Jamii uliboreshwa (ICHF).

Walisema ukosefu wa dawa badala ya kuwa msaada kwa wanachi kwamba waokoe maisha yao, lakini hali imezidi kuwa mbaya, kwa kuwa dawa hakuna na mwisho wengi wanakufa.

Walitoa mfano wa mtu mwenye bima kuandikiwa dawa anapokwenda kwenye dirisha hapati dawa yoyote na kutakiwa kusafiri umbali mrefu kupata dawa kwenye maduka rasmi yanayopokea bima jambo linalomfanya kutumia gharama kubwa na wakifika kwenye maduka wanakosa dawa husika.

Walitaka serikali kuliangalia suala hilo kwa kuwa afya za watu ni muhimu sana, vinginevyo itakuwa ni kupoteza nguvu kazi ambayo inatengenezwa kwa gharama kubwa.

Aidha, walisema kuna watu wanalazwa chumba cha wagonjwa mahututi (ICU), lakini bado hakuna dawa, jambo ambalo ni tishio kwa afya endelevu na nguvu kazi ya taifa.

Kilio dhidi ya huduma duni za dirisha maalum la kuhudumia wazee ni kilio cha muda mrefu, ambacho hata kwenye mkutano wa Rais Samia Suluhu Hassan na wazee wa Dar es Salaam kiiibuka na aliahidi mkakati madhubuti kuhakikisha huduma na upatikanaji wa dawa kwa kundi hilo.

Pia kundi la wajawazito kutozwa fedha huku mbunge mmoja akieleza ipo hospitali akizaliwa mtoto wa kiume ni Sh. 50,000 na wa kike ni Sh. 40,000, na kutaka serikali kusema kama huduma hizo ni bure au kuna malipo.

Pia huduma bure kwa watoto nayo ni changamoto kubwa ambayo ni ya muda mrefu nayo imekuwa kilio, na vyote vinachangia kuongeza vifo vya mama na mtoto.

Licha ya jitihada na changamoto nyingi za kibajeti, ni muhimu sana serikali ikatoa kipaumbele cha pekee kuhakikisha dawa zote muhimu zinapatikana hadi ngazi ya zahanati.

Pia hatua madhubuti zichukuliwe kwa wanaoiba dawa, wanaouza dawa kwenye maduka binafsi ambazo zimeshaharibika, kiasi cha kuongeza madhara makubwa ya afya ikiwamo magonjwa yasiyoambukiza.

Kilio hiki ni cha muda mrefu na hasa maeneo ya vijijini, kiasi cha watu ambao hawakustahili kufa wamekufa kwa kuwa tu huduma za afya siyo za kuridhisha na hasa kupata dawa za kutibu magonjwa au kupunguza maumivu.

Lazima serikali kupitia mifumo yake kuziba mianya yote ya upotevu wa dawa, ambayo linagusa na kuumiza wengi na hasa kuzingatia kuwa suala la afya ya mtu siyo la mjadala.

Bila hatua madhubuti, kila bajeti kilio kitajirudia, wananchi wengi wataumia kwa kuwa tu kuna ambao hawakuwajibika. Lazima uwekwe utaratibu sahihi wa zahanati, vituo vya afya na hospitali kupata dawa sahihi, kwa wakati katoka Bohari Kuu ya Dawa (MSD).

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Muhimu kuwapo sheria inayobana watoto wasiolea wazazi makusudi

Na Yasmine Protace

**KILA** anayeletwa duniani, ni zao la wazazi wawili. Hivyo, hao waliochangia uzazi huo, wana wajibu wa msingi kuwalea kwa nafasi yote.

Hata hivyo, kumekuwapo baadhi ya watu wasiokuwa tayari kutimiza hilo la malezi, katika sura ya pili pale wazazi wanapofika hatua sasa nao wamechoka kiafya, hawamudu tena badala ya kubeba jukumu kuwachukua na kuwasaidia kuwahudumia, eti wanathubutu kuwapeleka katika kambi ya malezi.

Kutokana na watu kushindwa kuwalea wazazi wao ambao wameshakuwa wazee sasa, wanaomba sheria zitungwe, ili wachukuliwe hatua watoto wao wenye uwezo wa kuhudumia wazazi, lakini wanawatekeleza.

Walesi Mwakikalo ni Mwenyekiti wa Wazee Kinondoni, anasema kuwa wao kutunzwa katika kambi ni kosa na haifai bali wanatakiwa kutunzwa na hata kujengewa nyumba au kulelewa na familia zao.

Anasema, tabia ya kubeba utamaduni wa kuwaweka wazee kambini na kuwaacha walelewa huko, si njema sana.

Anasema wazee wanaoishi kambini wanakuwa mara nyingi wanasumbuliwa na maradhi kama ya ukoma, upofu na matende.

Pia cha ajabu ni kwamba, kuna watu wanawapeleka hata wazee wasiokuwa na matatizo ya kiafya, katika makazi yao, eti kisa wamezeeka wakasaidiwe huko. Hiyo siyo sahihi hata kidogo.

Anasema, hadi sasa inafaa sheria zitungwe na ikiwezekana kuwapo namna ya kushinikiza watoto kugharamia matunzo ya wazazi, hata kupitia mishahara yao hao walioko kazini.

Ni mtazamo chanya kuungana mkono na Mzee Walesi, anayemshukuru Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kukutana nao na kujenga hoja chanya ya kuwasaidia.

Msingi mara zote, chanzo cha watoto kushindwa kufuatilia mmomonyoko wa maadili na hata wasiwasaidie wazee wao waliowazaaa, kuwasomesha, lakini bado kunachosikitisha mzazi asipompeleka mtoto shule, anachukuliwa hatua.

Mtoto akishindwa kumlea mzee, naye hachukuliwi hatua na hakuna sheria stahiki inayosimamia hilo kokote. Tujiulize, kama mzazi asipompeleka mtoto shule anachukuliwa hatua gani? Inajulikana kote, hatua kali huwa zinafuata.

Niliwasikia wazee hao katika siku yao kwa hatua kubwa wakiishukuru serikali kuwajali, hata wanapoenda hospitali wanapata matibabu stahiki, ingawa katika sura ya pili kunashuhudiwa hasa katika kupatikana vipimo na dawa pasipo pesa wanakwama.

Pia namkumbuka Mwenyekiti wa Baraza la Wazee Mkoa wa Dar es Salaam, Sakumu Matibwa, anasema kuwa jamii wajibu wao ni kuleta fadhila kwa wazazi.

Anasema, mmomonyoko wa maadili umechangia vijana kutokea wazee wanalalamika kutekelezwa na watoto wao, akifafanua: "Nchi za Ulaya Wazee kuishi kambini ni sawa lakini sio Tanzania."

Matibwa anaongeza makambi yanatakiwa yawahudumie wazee ambao hawajabahatika kuoa wa kuwa na watoto na sio, katika kambi anapelekwa mtu aliye na watoto.

Anasema, wapo baadhi ya vijana wanawatelekeza wazazi wao kutokana na kuishi mataifa ya Ulaya na kuoa huko na kushindwa kurudi kuwasaidia wazazi wao.

Matibwa anasema wazee wana sifa kuu tatu kusinzia, unafahamu na gadhabu, sasa wakiyafanya hayo wasilaumiwe na kushindwa kuwasaidia wazazi.

Wazee wanaathirika, pale alipokuwa na kazi na akistaafu anapewa mafao na kuoa nyumba ndogo, hapo unakuta changamoto inatokea na watoto kumchukia baba.

"Watoto wanatakiwa kuwa karibu na wazazi, hata anapopata kiinua mgongo, anasaidia utunzaji fedha na ikiwezekana anajengewa nyumba ili imsaidie," anasema.

Msingi wa hoja ni kwamba, watoto wanapowatunza wazazi wao, inasaidia hata serikali kupunguza gharama za kuwalea wazee na kuwajengea nyumba za kuwatunza.

Ushauri mkuu ni wazee watunzwe nyumbani kwao, kwa kuwa ni hatua yenye faida yake, mojawapo akitaja kuwa ni mzee huyo kuwa mlezi wa familia na hata mjukuu wake atakuwa anamwangalia vyema, kwa msaada wa ushirikiano wa dada wa kazi au vinginevyo.

## HABARI KITAIFA




Katibu Tawala wa Mkoa wa Lindi, Rehema Madenge, akipokea zawadi ya mzani kutoka kwa Meneja wa Wakala wa Vipimo (WMA) mkoa wa Lindi, Andrew Mbwambo, baada ya kufungua mkutano wa elimu kwa umma inayotolewa na wakala huo, mkoani humo juzi.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mume ashikiliwa madai kuua mke

**Na Said Hamdani,** LINDI

MKULIMA wa Kijiji na Kata ya Mandawa, Wilaya ya Kilwa mkoani Lindi, Said Mohamedi Nanguwili (49), anashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma za kumuua mkewe Rafa Omari (40).

Chanzo cha mauaji hayo kimeelezwa kuwa ni ugomvi unaodaiwa kutokana na wivu wa kimapenzi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyothibitishwa na Kamanda wa Polisi mkoani hapa, ACP Mtatiro Kitinkwi, mauaji hayo, yanadaiwa kufanywa Mei 11, mwaka huu.

Kitinkwi alisema mtuhumiwa na mkewe kwa muda mrefu hawakuwa na maelewano mazuri kwenye nyumba yao, hali iliyosababisha Rafa kuuawa na mumewe.

Alisema mwili wa mwanamke hiyo ulikutwa na watu waliokuwa wakipita njia maeneo ya porini karibu na mashamba ya mpunga, huku ukiwa umevunjwa shingo.

"Mwili wa Rafa umekutwa na watu waliokuwa wakipita njia ukiwa umetelekezwa porini karibu na maeneo ya mashamba ya mpunga," alisema.

Kitinkwi alisema tayari mtuhumiwa Nanguwili amekamatwa na mwamba anaendelea kuhojiwa na Polisi na baada ya mahojiano na upelelezi kukamilika, watampeleka mahakamani.

# Waziri ataka wenye hati za kimila wapate mikopo

**Na James Mwanamyoto,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mohamed Mchengerwa, amezitaka taasisi za kifedha nchini kutoa mikopo kwa wananchi wenye hatimiliki za kimila zinazotolewa na Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) ili kuwawezesha wananchi hao kuendesha shughuli zao na kuinua kipato.

Akikabidhi hatimiliki hizo kwa baadhi ya wananchi wa Shehia ya Welezo, Zanzibar jana, Mchengerwa alisema hatimiliki hizo zinalenga kutoa fursa kwa wananchi kupata mikopo itayowawezesha kufanya shughuli mbalimbali ikiwamo kilimo na biashara ili kuboresha maisha yao.

"Taasisi za kifedha zitambue hatimiliki hizi na kupunguza masharti ili kuwawezesha wafanyabiashara wadogo kukopa na kuongeza mtaji," Mchengerwa alisisitiza.

Akiwa katika Kituo Jumuishi cha Urasimishaji na Uendelezaji Biashara kilichoko katika Baraza la Biashara, eneo la Darajani Wilaya ya Mjini, Mchengerwa alizitaka taasisi za kifedha kutoa mikopo kwa wajasiriamali waliorasimisha biashara zao na kuongeza kuwa, mikopo hiyo itawaongezea mitaji ya kuendesha shughuli zao za ujasiriamali.

Kutokana na uwapo wa kituo hicho, Mchengerwa alihimiza urasimishaji biashara usichukue muda mrefu ili kutoa hamasa kwa wananchi kujitokeza kwa wingi kurasimisha biashara zao.

Katibu Mkuu Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar, Dk. Islam Seif Salum, alisema kituo hicho kimejengwa ili kuondoa kero za urasimishaji walizokuwa wakikutana nazo wafanyabiashara wadogo.

Dk. Salum serikali imedhamiria kujenga kituo kama hicho Pemba ili wananchi wa eneo hilo nao wanufaike.

Mratibu wa MKURABITA, Dk. Seraphia Mgembe, alisema utekelezaji wa MKURABITA Zanzibar umewanufaisha wananchi wa Zanzibar kwa kuwapatia mafunzo ya utunzaji wa kumbukumbu za biashara ambapo hivi sasa wanazo takwimu sahihi za maendeleo ya biashara zao.

Mchengerwa alihitimisha ziara yake ya kikazi Zanzibar ya kukagua miradi inayotekelezwa na taasisi zilizo chini ya ofisi yake ikiwa ni pamoja na kuhimiza uwajibikaji kwa watumishi wa Sekretarieti ya Ajira Ofisi ya Zanzibar.

# 'Marufuku kutoza fedha za matibabu watoto chini miaka 5'

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MKUU wa Wilaya ya Njombe, Ruth Msafiri, ameagiza kituo cha afya Makambako kuacha mara moja kuwatoza fedha za matibabu watoto chini ya umri wa miaka mitano kwa kuwa ni kinyume na sera ya afya.

Akizungumza na Nipashe jana ofisini kwake kutokana na malalamiko ya baadhi ya wananchi wa Halmashauri ya Mji wa Makambako kutozwa Sh. 4,000 kwa ajili ya matibabu ya watoto walio kwenye umri huo, Mkuu wa Wilaya alisema sera ya afya inataka mtoto chini ya miaka mitano kutibiwa bure na wanapaswa kutekeleza sera hiyo kikamilifu.

"Tayari mtoto chini ya miaka mitano anamsamaha, hata katika bima iliyoboreshwa kimsingi hayumo," alisema Msafiri.

"Hatua hizo za Makambako siziungi mkono hata kidogo, pia nazikataa kwasababu walishawahi kuja kuniambia kwamba wamefuta basi wasirudie na sio sahihi kumchukua mtoto na kumwambia utakuja kwa rufani," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Makambako, Hanana Mfikwa, alikiri kuwapo kwa tatizo hilo kutokana na mkanganyiko uliojitokeza baada ya ujio wa Naibu Waziri TAMISEMI, Dk. Festo Dugange, pamoja na mwongozo wa serikali na kuuondoa utaratibu wa kulipia watoto chini ya miaka mitano, wajawazito na wazee wasiojiweza.

"Ni kiri kwamba tatizo hili tulifuatilia tuliona lilikuwapo, kwa hiyo watoto, wajawazito na wazee hawataendelea kutozwa na mpaka sasa zoezi hilo limesimamishwa kwa watoto kuanzia mwaka sifuri mpaka mitano wanatakiwa wapate huduma hii ya afya bure, lakini wazazi wazingatie kwenda na kadi ya kliniki," alisema Mfikwa.

Hata hivyo, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Makambako, Paul Malala, aliwataka wananchi kuzitumia zahanati zilizojengwa katika kata za maeneo yao badala ya kutembea umbali mrefu kufuata huduma za afya katika kituo cha afya Makambako.

"Tuna ngazi mbalimbali za upataji wa huduma za afya kuanzia zahanati, kituo cha afya na kuendelea na kilichokuwa kinafanyika ni kuwaelewesha wazazi tu namna ya kupata huduma za afya," alisema Malala.

Baadhi ya wananchi wa mji huo wameishukuru serikali kwa kuwarejeshea utaratibu wa matibabu bure kwa watoto walio chini ya umri wa miaka mitano kwa kuwa imewapunguzia mzigo wa wazazi.

# SMZ yatambua mchango wadau mapambano VVU

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) imesema inatambua mchango unaotolewa na taasisi za dini pamoja na wadau wa maendeleo Zanzibar katika mapambano dhidi ya Virusi vya Ukimwi (VVU) na Ukimwi katika kuweka mazingira wezeshi kwa wananchi kupata elimu hiyo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Ukimwi Zanzibar (ZAC), Dk. Ahmed Mohammed Khatib, alitoa kauli hiyo jana katika uzinduzi wa machapisho ya uhamasishaji wa wanaume na watoto kutumia huduma za VVU na Ukimwi kupitia taasisi za kidini.

Alisema taasisi za dini zimekuwa na mchango mkubwa katika mafanikio yaliyofikiwa katika mwitikio wa kitaifa nchini katika kupambana na ugonjwa huo.

Alibainisha kuwa hadi kufikia Desemba mwaka jana, Zanzibar ilifikia malengo ya 90,90,90 ikiwa 92 kwa 90 ya mwanzo 99 kwa 90 ya pili na 93 kwa 90 ya tatu, yaani 92,99,90.

Mkurugenzi huyo alisema mafanikio hayo yamepelekea kupunguza maambukizo mapya na vifo vitokanavyo na Ukimwi, hivyo anaamini kuna mchango mkubwa wa taasisi za dini hasa katika kutoa elimu na huduma kwa jamii kwa haraka na uhakika.

Alisema kwa Zanzibar, takwimu zinaonyesha kwa sasa kuna asilimia 0.4 ya Wazanzibari ambao wanaishi na VVU kulinganisha na asilimia moja kwa mwaka 2012.

Hata hivyo, alibainisha kuwa hadi kufikia Machi mwaka huu, kulikuwa na watu 8,147 wanaopata huduma katika vituo vya huduma kwa watu wanaoishi na VVU. Kati yao, wanaume ni 2,526 na wanawake 5,621 na asilimia nne ni watoto wenye umri wa miaka 14 ambao ni 292.

Alisema pamoja na mafanikio hayo, utafiti wa viashiria vya VVU na Ukwimu (THIS) wa mwaka 2016/17 ulionyesha bado kuna maeneo yenye upungufu yanayotakiwa kufanyiwa kazi kwa haraka na ushirikikiano wa wadau wote, zikiwamo taasisi za dini.

Aliyataja kuwa ni pamoja na wanaume na watoto kuwa nyuma katika upimaji wa VVU, uanzaji wa dawa za ARV na ufuasi endelevu wa dawa hizo.

Alibainisha kuwa takwimu za 2016/17 zilionyesha kuwa asilimia 41 ya wanaume wanaoishi na VVU hawajawahi kupima VVU nchini, hivyo hawajui hali zao, lakini wanaojijua wana tatizo la kuanza dawa mapema au kutokunywa dawa, hivyo hupelekea kuongezeka vifo vinavyotokana na Ukimwi na VVU.

"Miongoni mwa vifo vinavyojitokeza vingi vinahusisha wanaume kuanzia umri wa miaka 15 ambao ni 12,000 hufariki kwa mwaka kulinganisha na wanawake, baadhi ya familia, wazazi wanaoishi na VVU hawajawapima watoto wao walio chini ya miaka 15 na kwa walezi wanaoishi na watoto wenye maambukizi ya VVU hawajawapeleka watoto hao kuanza huduma za tiba na matunzo kwa ustawi wao," alibainisha.

Alisema tatizo lingine kuwapo kwa unyanyapaa kwa watu wanaoishi na VVU (WAVIU) hali inayokatisha tamaa baadhi ya wananchi kupima VVU na kuanza huduma za matibabu kwa wakati.

Sambamba na hayo, alisema ili kuwafikishia huduma wananchi, serikali kupitia ZAC ina jukumu la kufanya kazi na wadau wote wanaotekeleza afua za VVU na UKIMWI Zanzibar na kutumia majukwaa mbalimbali kutokana na uwezo walionao katika kuifikia jamii kwa urahisi ikiwemo tasisi za kidini kupeleka habari na ujumbe mpya kwa jamii juu ya huduma za upimaji wa VVU, matibabu mapya na kuibua mijadala inayolenga kuleta mabadiliko chanya ya tabia ili kupunguza maambukizi mapya.

Akitoa salamu kutoka Ofisi ya Mufti Zanzibar, Mkurugenzi Utawala na Rasilimali Watu, Shekh Othman Mohammed Saleh, alipongeza serikali kupitia taasisi zake ikiwamo ZAC na Wizara ya Afya kwa kushirikiana na tasisi za dini kwa kuwa ni muhimu katika kufikisha ujumbe kwa urahisi.

Alisema machapisho hayo yamekuja wakati mwafaka hasa kufikia lengo la serikali kumaliza Ukimwi na VVU ifikapo mwaka 2030.

Meneja Msaidizi wa Kitengo Shirikishi Ukimwi, Homa ya Inni, Kifua Kikuu na Ukoma kutoka Wizara ya Afya Zanzibar, Issa Abeid Mussa, alisema Ukimwi huathiri wanaume na watoto pekee, bali unaathiri watu wengi ulimwenguni.

## Shule ya watoto wenye ulemavu yakabiliwa upungufu walimu maalum

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

SHULE ya Msingi Buhangija Jumuishi, iliyopo Manispaa ya Shinyanga, inayotoa elimu kwa watoto wenye ulemavu wa aina mbalimbali inakabiliwa na upungufu wa walimu maalum.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Fatuma Jilala, alibainisha hayo juzi wakati akizungumza na Nipashe ilipotembelea shuleni hapo.

Alisema shule hiyo ina jumla ya wanafunzi 1,049, na kati ya hao wenye ulemavu ni 227 na waliopo ni 19.

"Kutokana na upungufu huo wa walimu maalum, tunapata shida kutoa elimu kwa wanafunzi hawa wenye ulemavu, ambapo walimu waliopo inabidi wapambane hivyo hivyo kuwafundisha bila ya kuchoka," alisema Jilala.

"Tunaomba serikali itupatie walimu wenye taaluma maalum, ili tuendelee kufanya vizuri kitaaluma, sababu shule inapokuwa na upungufu wa walimu hawa, tunapata shida sana katika ufundishaji kulingana na hali zao," aliongeza.

Ofisa Elimu shule za msingi Manispaa ya Shinyanga, Neema Mkanga, alisema tayari serikali imeshaomba walimu wenye taaluma maalum wizarani, huku akitoa wito kwa walimu kuendelea kufundisha kwa bidii watoto hao ili wafaulu na kutimiza ndoto zao.



Mkuu wa Shule ya Awali Feza, Arzu Yilmaz (wa tatu kushoto), akikata keki kuadhimisha Siku ya Kinamama Dunia pamoja na wazazi wa watoto shuleni hapo, Mikocheni, jijini Dar es Salaam mapema wiki hii. **PICHA: ASHIRACK MIRAJI**

# Mbunge kuufikisha mgogoro wa ardhi kwa Waziri Lukuvi

**Na Richard Makore,** MBOGWE

MBUNGE wa Mbogwe, Nicodemus Maganga, ameahidi kufikisha kwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, mgogoro wa wachimbaji wadogo katika eneo la Nyakafuru mkoani Geita.

Mgogoro huo wa ardhi ulisababisha wakulima 200 kukimbia mashamba yao.

Akizungumza na Nipashe jana katika Wilaya ya Mbogwe, kuhusu mgogoro huo, Maganga alisema amepata vielelezo vya wakulima hao na kwamba atafikisha suala hilo kwa Lukuvi.

Alisema sheria ya ardhi ipo wazi kwamba wakulima hao walitakiwa kupata mgao wa asilimia 15 na serikali asilimia 15.

Aliongeza kuwa kikundi cha Isanjabadugu kilivamia mashamba hayo ya wakulima na kuanzisha uchimbaji wa dhahabu mwaka 2017.

Maganga alisema kumekuwa na mgogoro katika eneo hilo kati ya wenye mashamba na kikundi hicho na kwamba atahakikisha anafuatilia mapato yanayopatikana katika machimbo hayo.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Nyakafuru' C', wilayani Mbogwe, Sandu Mboje, alisema mgogoro huo umewanyima haki wakulima hao.

Alisema mgogoro huo ulianza mwaka 2017 baada ya kikundi hicho kuvamia mashamba hayo na kuanza shughuli za uchimbaji wa dhahabu.

Makamu mwenyekiti wa kikundi cha Isanjabadugu, Mastula Samuel, alisema walianza shughuli za uchimbaji tangu mwaka 2017.

Alisema wao hawataki kuwa na mgogoro na wamiliki wa mashamba ambao waliwakuta, na kwamba kwa sasa wanafanya shughuli zao bila leseni.

# Mbunge ataka uchunguzi wa mtambo wa barakoa wa MSD

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Viti Maalum, Agnesta Kaiza, ameiomba serikali kufanya uchunguzi wa kina kuhusu mtambo wa kutengeneza barakoa ulionunuliwa na Bohari ya Dawa nchini (MSD), kutokana na kutofanya kazi kwa ufanisi.

Akichangia bungeni jana makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka 2021/22, Kaiza alisema mtambo huo ulinunuliwa kwa dharura na kuigharimu serikali zaidi ya Sh.milioni 600 lakini unazalisha kwa kiwango cha chini.

Alisema mtambo huo ulitakiwa kuzalisha barakoa milioni nne kwa mwezi, lakini hadi Septemba mwaka jana ulizalisha barakoa 320,000.

"Mpaka sasa mtambo huu umezalisha asilimia nne ya uwezo wake. Naiomba Serikali ifanye uchunguzi wa kina kuhusiana na ununuzi wa huo mtambo wa kutengeneza barakoa wa MSD, tumenunua kwa pesa nyingi lakini cha kushangaza mtambo huo umekuwa ukizalisha chini ya kiwango," alisema.

Aliongeza: "Baada ya mtambo huo kuja ukaonekana 'compressor' iliyokuwapo haikuwa na nguvu ya yakuzalisha barakoa milioni nne kwa mwezi jambo lililopelekea uongozi kukubaliana mtambo huo uzalishe barakoa 504 kwa mwezi, lakini hata hiyo haikuwezekana kwani matokeo yake unazalisha chini ya lengo."

Alisema MSD imeiangusha serikali katika hilo licha ya serikali kusisitiza watu wavae barakoa zinazozalishwa hapa nchini kwa ajili ya uhakika wa afya zao.

" Hii inaonekana tumeuziwa mbuzi kwenye gunia, haiwezekani mtambo ununuliwe kwa pesa nyingi alafu matokeo yake uzalishe kwa kiwango cha asilimia nne tu,"alisema.

Aliitaka serikali kulipa deni la Sh. billioni 256 wanalodaiwa na MSD ili kuagiza dawa.

Alisema serikali imekuwa mdaiwa sugu wa MSD, kwamba bajeti iliyoidhinishwa mwaka 2019/20 ilikuwa Sh. bilioni 200, lakini Serikali haikupeleka fedha.




Ofisa Mkuu wa Rasilimali Watu Benki ya NMB -Emmanuel Akonaay (mwenye miwani), akiwa na Meneja wa Kanda ya Dar es Salaam, Donatus Richard pamoja na watoto wa kituo cha yatima cha Ijango Zaida kilichoko Sinza Madukani, baada ya kutoa msaada wa vyakula kwa ajili ya sherehe za Eid el Fitr. Benki ya NMB jana ilitoa mkono wa Eid kwa vituo 12 nchini ili kuwezesha watoto zaidi ya 1,000 kusherehekea sikukuu ya Eid el Fitr.

# Kampuni 54 kushiriki Sabasaba

**Na Maulid Mmbaga**

WIZARA ya Viwanda na Biashara kupitia Taasisi yake ya Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade), inaandaa maonyesho ya 45 ya biashara ya kimataifa yanayotarajiwa kufanyika jijini, yakishirikisha kampuni 54.

Maonyesho hayo yanatarajiwa kufanyika mkoani Dar es Salaam kuanzia Juni 28 hadi Julai 13, 2021.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na mamlaka hiyo, lengo la maonyesho hayo ni kutoa fursa kwa wafanyabiashara wa ndani na nje ya nchi pamoja na taasisi mbalimbali kutangaza biashara ya bidhaa na huduma, kujifunza uzalishaji bora wa bidhaa kulingana na soko la kimataifa.

Lengo lengine ni kutengeneza mtandao wa mawasiliano baina ya wafanyabiashara utakayowasaidia kukuza biashara na kupata wabia kwenye biashara zao ili kuweza kufikia malengo waliyojiwekea.

"Kauli mbiu ya maonyesho ya mwaka huu ni 'Uchumi wa Viwanda kwa Ajira na Biashara Endelevu' kauli mbiu hii inalenga kutambua mchango wa sekta ya viwanda katika kuchochea uzalishaji kwenye sekta mbalimbali za kiuchumi ili kukuza biashara ya ndani na nje, kuongeza ajira na hivyo kuchangia katika ukuaji wa uchumi wa taifa," ilisema.

Nchi zitakazoshiriki ni China, Ghana, Kenya, Pakistan, Syria, India na Umoja wa Falme za nchi za Kiarabu (UAE), huku kampuni zipatazo 54 kutoka nje ya nchi na 2,803 za ndani ya nchi zikithibitisha kushiriki.

Pia sambamba na maonyesho hayo, itafanyika mikutano ya kibiashara (B2B) kwa njia ya mtandao ili kuwakutanisha wadau wa ndani na nje ya nchi kwa lengo la kutafuta masoko ya bidhaa na huduma zinazozalishwa nchini yakiwamo mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi, misitu na madini.

# Kortini kwa tuhuma za kusafirisha heroin

**Na Hellen Mwango**

WATU 11 akiwamo mfanyabiashara, Silvanus Mkasanga, wamefikishwa mahakamani wakikabiliwa na tuhuma za kusafirisha kilo 20.24 za dawa za kulevya aina ya heroin.

Wengine ni Ally Juma, Rifat Omary, Haruna Salu, Godlisten Mamba, Flora Mamba, Khamis Khamis, Yuda Muhagama, Justine Mnyalape, Emmanuel Mgeni na Mikidadi Nyangale.

Walisomewa shtaka lao katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Yusto Luboroga.

Wakili wa Serikali, Yusuph Aboud, alidai kuwa Aprili 29, mwaka huu, eneo la Sangasanga Check Point, Wilaya ya Mvomero, Mkoa wa Morogoro, washtakiwa walikutwa wakisafirisha dawa za kulevya zenye uzito huo.

Upande wa Jamhuri ulidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika na kuomba tarehe nyingine ya kutajwa.

Hakimu Luboroga aliamuru washtakiwa wapelekwe rumande mpaka Mei 26, mwaka huu.

# Mkakati wa kuikabili malaria wapata nguvu

**Na Enock Charles**

KATIKA kupambana na malaria nchini, Kampuni ya Kansai Plascon imezindua bidhaa zake mpya ikiwamo rangi ya Plascon Anri Mosquito Paint yenye uwezo wa kuua mbu muda mfupi baada ya kutua ukutani.

Hatua hiyo hupunguza uwezekano wa wenye nyumba kuugua malaria, huku ikimtambulisha Lucas Mhuvile almaarufu Joti kuwa balozi wa rangi hiyo nchini.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni hiyo, Hussein Jamal, alisema walibuni bidhaa hiyo ili kupunguza kiwango cha malaria katika mataifa ya Afrika ikiwamo Tanzania ambapo bado malaria ni tishio kubwa.

"Plascon Anti Mosquito Paint ni rangi mpya kabisa na ni ya kwanza Tanzania yenye uwezo wa kuua mbu muda mfupi baada ya kutua ukutani ... rangi hii Plascon imeileta ili kusaidia Tanzania kuondoa malaria," alisema Jamal.

Balozi wa rangi hiyo Lucas Mhuvile alisema licha ya rangi hiyo kuua mbu, lakini haina madhara kwa binadamu ila imewekewa sumu ya kiwango cha kuua mbu pekee na kupunguza uwezekano wa kuweka vyandarua vingi ndani ya nyumba .



Mkurugenzi Mkuu wa Kituo cha Uwekezaji (TIC), Dk. Maduhu Kazi (kushoto), akifafanua kuhusu kituo kipya cha mawasiliano kwa wawekezaji kilichoanzishwa na TIC, jijini Dar es Salaam juzi. Kulia ni Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Prof. Godius Kahyarara na Isack Mbena kutoka Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF). **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Kituo cha mawasiliano kwa wawekezaji chaanza

**Na Josseph Mwendapole**

KITUO cha Uwekezaji (TIC), kimeanzisha kituo cha mawasiliano kwa wawekezaji, ikiwa ni hatua ya kupunguza usumbufu.

Usumbufu huo ni wa kusafiri umbali mrefu kwenda kutafuta taarifa za uwekezaji kwenye kituo hicho. Uzinduzi wa kituo hicho ulifanywa jana na Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Prof. Godius Kahyarara, jijini Dar es Salaam akiwa na Mkurugenzi wa TIC, Dk. Maduhu Kazi.

Prof. Kyarara alisema kuanzishwa kwa kituo hicho ni sehemu ya maboresho yanayofanywa kwa ajili ya kuboresha mazingira ya uwekezaji.

Alisema nia ya TIC kuanzisha kituo hicho ni kuwawezesha na kuwarahishia wadau wa uwekezaji kupata taarifa wanazohitaji kwa njia ya kupiga simu, barua pepe na mitandao.

Alitaja huduma zinazopatikana kwenye kituo hicho ni za fursa za uwekezaji zilizopo nchini na taratibu za kuwekeza pamoja na kupata leseni na vibali.

Zingine ni kutoa ushauri kuhusu sera, sheria na taratibu zinazohusu uwekezaji nchini na wawekezaji kupata taarifa za maendeleo ya maombi yao ya vibali na leseni waliyowasilisha kwa TIC.

Alitaja faida ya kuwapo kwa kituo hicho kuwa ni kupunguza muda na gharama kwa wawekezaji kwani badala ya kufika TIC watakuwa wanapata huduma hizo kupitia kituo hicho wakiwa popote ndani na nje ya nchi.

Aidha, alisema kituo hicho kitasaidia kuondoa taarifa potofu walizokuwa wanapata wawekezaji kutoka vyanzo mbalimbali ambavyo si sahihi.

# Wakuu asasi za kiraia waijadili ripoti ya CAG

**Na Mary Geofrey**

JUKWAA la Wakurugenzi wa asasi za kiraia nchini, wamekutana kujadili Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya mwaka wa fedha 2019/2020 kwa lengo la kuboresha utendaji kazi.

Mkutano huo umefanyika ili kupata uchambuzi wa taarifa hiyo na kuchukua hatua za kuboresha uwajibikaji na uwazi katika utendaji kwa serikali.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Civil Society (FCS), Francis Kiwanga, iliyoandaa mkutano huo kwa kushirikiana na WAJIBU Institute of Public Accountability, akizungumza wakati wa kuufungua jana jijini Dodoma, alisema wamekuwa wakifanya hivyo kwa ajili ya kusaidia katika masuala ya uwazi na uwajibikaji.

"Kila mwaka huwa tunakutana kujadili taarifa za ukaguzi wa hesabu za serikali lengo likiwa ni kuongeza nidhamu na kudhibiti ubadhirifu wa rasilimali za serikali na kupitia majadiliano haya tutakuwa na jambo moja katika kuimarisha utendaji kazi wetu," alisema Kiwanga.

Aliongeza kuwa kama asasi za kiraia wamekuwa wakifanya kazi na serikali ili kuwasaidia wananchi katika suala la uwazi na uwajibikaji kwa maslahi mapana ya nchi.

Akizungumza wakati wa kuwasilisha mada kwenye mkutano huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya WAJIBU, Ludovick Utouh, alisema taasisi yake ndiyo iliyofanya uchambuzi wa ripoti hiyo na kwamba wanampongeza CAG Charles Kichere, kwa ripoti hiyo nzuri yenye jumla ya ripoti 21.

Utouh ambaye ni CAG Mstaafu, alisema kumekuwapo na suala la kuongezeka kwa hati chafu.

Alisema suala hilo linaonyesha kuna shida katika suala la hesabu hasa udhaifu katika kaguzi za ndani.

Aidha, aliwataka wananchi kuhakikisha wanaimarisha masuala ya uwazi na uwajibikaji katika kuikosoa serikali.

# NMB yazawadia yatima Eid el Fitri

**Na Mwandishi Wetu**

WATOTO yatima 1,000 katika vituo 12 nchini, wamepatiwa msaada ikiwa ni zawadi ya Eid el Fitri.

Uwezeshaji huo umefanywa na Benki ya NMB kwa vituo vya kanda zote za benki hiyo nchini wamefikiwa na msaada huo.

Akizungumza katika Kituo cha Watoto Yatima Ijango Zaidia kilichopo Sinza jijini Dar es Salaam, baada ya kukabidhi msaada huo, Ofisa Mkuu wa Rasilimali Watu Benki ya NMB, Emmanuel Akonaay, alisema Mwezi Mtukufu wa Ramadhani umewakumbusha watu umuhimu wa kutoa kwa wanaomzunguka hasa wasiojiweza kwa kipato.

"Sisi Benki ya NMB tunatambua Mwezi Mtukufu wa Ramadhani unaowagusa zaidi ya Waislamu bilioni 1.5 ulimwenguni ambao miongoni mwao kuna wafanyakazi wenzetu, wateja wetu, wabia, wawekezaji na wanahisa. Mwaka huu tumeona vyema zaidi kujumuika na watoto wa vituo vya yatima nchini kutoa sadaka hii ya mkono wa Eid," alisema Akonaay na kuongeza:

"Dini zote, Waislamu kwa Wakristo tuna imani kuwa Mola humsaidia mtu anayemsaidia ndugu yake. Kwa maneno mengine ni kwamba, tumeumbwa ili tuwasaidie wengine na hili ndilo kusudi la uwepo wetu hapa kwenye kituo hiki cha watoto yatima cha Ijango Zaidia cha Sinza Madukani jijini Dar es Salaam."

Aidha, ofisa huyo alibainisha kuwa sadaka hiyo ya mkono wa Eid itafanywa pia na wafanyakazi wengine wa benki hiyo kwenye kanda zote nchini kutoa vyakula mbalimbali vikiwamo mbuzi, mchele, mafuta ya kupikia, sukari, majani ya chai, pamoja na vifaa vingine vya kupikia kwa ajili ya watoto kupata mlo wa sikukuu.

Mkuu wa Kituo cha Watoto Yatima, Ijango Zaidia, Zaidia Nuru, alisema: "Mlichofanya ni kitu kikubwa kwa watoto hawa. Hawana wazazi sisi na nyinyi ndio wazazi wao. Hakika Mungu atawalipa kwa kila mlichotoa mkafanikiwe zaidi kwenye shughuli mnazofanya."


Meneja wa Kanda ya Dar es Salaam na Zanzibar, Donatus Richard, alisema kuwapa tabasamu wanajamii ni sehemu ya utamaduni wa benki hiyo.

Sheikh wa Wilaya ya Tabora, Ramadhani Juma ambaye alishiriki hafla ya makabidhiano kwa Kanda ya Magharibi, alisema NMB imeonyesha mfano wa kuigwa, mashirika, taasisi na watu binafsi wanatakiwa kuguswa kusaidia watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu wakati wote.



Ukurasa 14

Wizara Kilimo, JKT waingia ubia wa uzalishaji kitaifa




Ukurasa 13

Tushirikiane kujenga demokrasia, uchumi



Ukurasa 12

**Wafanyabiashara kutoka soko kuu Tarime walivyobaki 'hoi' walikohamishwa kwa muda**

BUFE
IJUMAA MEI 14, 2021
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

## KIKUNDI CHA JIPE MOYO

# Kinamama wakulima wa mfano waliowainua vitini DC na mbunge

• Hamasa kuwaiga, vyazaliwa vikundi 15

**Na Sabato Kasika**

KILIMO kimo katika kundi la wanaoingizia serikali fedha nyingi za kigeni, pia kikiajiri takriban theluthi mbili ya Watanzania wote.

Hadi sasa, kilimo ambacho muumini wake mkuu Hayati Mwalimu Julius Nyerere alikibatiza kuwa 'uti wa mgongo wa taifa' kimepitia hatua nyingi za kimaendeleo, kitaifa na kimataifa.

Mojawapo ni katika kuanzishwa vikundi vya maendeleo ya kilimo na kinamama kama kawaida yao, hawako nyuma, huku Rais wa sasa Samia Suluhu Hassan, akiwa wazi anawahimiza kunyanyuka 'kifua mbele.'

Ndani ya mustakabali huo, ukiakisiwa moja kwa moja kutoka ukingoni mwa Ziwa Victoria, katika kijiji cha Kome Kata ya Bwasi, ndani ya Hamlashauri ya Musoma Vijijini, mkoani Mara, kuna kikundi cha kilimo cha kinamama kiitwacho Jipe Moyo, chenye jumla ya wanachama 35.

Katibu, Deborah Isaack, anasema wana bustani za kuzalisha matikiti maji, nyanya, vitunguu na kabichi, chanzo kikuu cha umwagilaji, ni maji ya ziwani Victoria.

"Pia, kwa kilimo kinachotegemea msimu wa mvua, tunalima mahindi, mihogo, maharagwe na alizeti ambayo ni jipya huku kwetu, ila linastawi kwa wingi," anasema Deborah.

Anasema Jipe Moyo ilianzishwa miaka saba iliyopita, ikiwa na wanachama 12, baada ya yeye kuwahamasisha kinamama wenzake kuungana kwa ajili ya kilimo cha bustani kando ya Ziwa Victoria.



Wanachama wa kikundi cha Jipe Moyo wakiandaa moja ya mashamba yao. **MPIGAPICHA WETU**

"Tulichangishana fedha na kupata Sh. 400,000 ambazo tulizitumia kununua mbegu za matikiti maji na vifaa vingine na kufanikiwa kupata Sh. 500,000, baada ya mavuno, ingawa lengo lilikuwa ni Sh. milioni moja," anasema.

Anafafanua kuwa fedha hizo walitumia kulima ekari moja ya mahindi na mihogo, pia wakapanua bustani kuongeza mazao ya nyanya, vitunguu, kabichi na mengine.

Ni hatua inayotajwa ya manufaa kuwaongeza mazao, mfuko wa kikundi ukatuna kila baada ya mavuno, sasa katibu huyo anajivunia wameongeza zao la biashara alizeti

"Wadau wa kilimo akiwamo Mbunge wa Musoma Vijijini, Prof. Sospeter Muhongo, alitusaidia jembe la kukokotwa na ng'ombe, pia kila mwaka amekuwa akitusaidia mbegu za mahindi, mihogo, mtama na alizeti," anasema.

Pia, Katibu Deborah, anasimulia shirika lisilo la kiserikali la Project Concern International (PCI), limewachangia mashine ya kumwagilia bustani.

Aidha, halmashauri wanakoishi ilishawakopesha Sh. milioni 12 za kuimarisha kikundi chao, kwa awamu mbili, akijigamba wamekuwa mfano wa kuigwa.

Utaratibu waliojiwekea, kila mwanachama ananunua hisa kuanzia moja hadi tano, kila hisa inauzwa Sh. 2,000 na kiwango cha kila mwanachama kukopeshwa, kinategemea hisa zake, kati ya Sh.100, 000 hadi Sh. 150,000.

### MIPANGO YAO

Deborah anataja mipango yao, inajumuisha kuongeza hisa za mfuko wa fedha za kukopeshana, kuotesha miti ya misitu na ufugaji nyuki kwa ajili ya biashara ya asali.

"Tunakusudia kuanzisha kiwanda cha kukamua mafuta ya alizeti, kwani kwa sasa tunatafuta eneo la kujenga jengo ambalo itawekwa mashine hiyo ambayo tumeahidiwa kupewa na PCI," anasema.

Pia, Katibu Deborah anasema azma yao ni kufikisha wanachama 50 na kununua mashamba ya kikundi, wakiachana na mfumo wa kukodi wanaotumia sasa. Hadi sasa benki wana akiba zaidi ya Sh. Milioni 10.

### WADAU MAENDELEO

Ofisa Kilimo wa Kata ya Bwasi, Alex Mihambo, anasema kikundi cha Jipe Moyo, kimewapa wakazi wengine wa Kijiji cha Kome, kuanzisha vikundi vya kilimo na jumla yao kuna vikundi 15.

"Ninachofanya kama Ofisa Kilimo, ni kuendelea kufuatilia shughuli za kilimo za kikundi cha Jipe Moyo na nitahakikisha kinapata soko la uhakika za mazao yake ndani na nje ya kata yetu," anasema Mihambo.

Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Dk. Vincent Anney, anasema mwitikio wa uanzishaji vikundi hivyo ni mzuri kwa kuiga mfano wa Jipe Moyo. Hadi sasa anashirikiana na viongozi wenzake, kuwashawishi wanavijiji majirani wa Musoma Vijijini,

"Vikundi vya kujikwamua kiuchumi si kwenye kilimo cha umwagiliaji, bali pia uvuvi wa samaki, ufugaji wa nyuki na shughuli nyingine za kuwaingizia kipato," anasema Dk. Anney.

Huku akiwapongeza wadau wengine wa kilimo wanaowapatia mbegu za mazao na umuhimu wa kuwahamasisha, anaendelea: "Tunataka wananchi watumie fursa zote za kiuchumi zilizopo kwenye maeneo yao, kwa ajili ya kujiletea maendeleo, hivyo suala la kuwahamasisha ni muhimu ili watambue fursa hizo."

BIASHARA

# Wafanyabiashara kutoka soko kuu Tarime walivyobaki ‘hoi’ walikohamishwa kwa muda

## • Mauzo ya siku; dagaa kilo 2; majiko mawili • Nyumbani kumudu kodi yabaki mtihani • Mkurugenzi awahakikishia neema yao iko njiani

**Na Anthony Gervas,** aliyekuwa TARIME

USEMI ‘maisha ni safari ndefu’ daima ni pana kwa jamii. Hilo likisogezwa kwa mfanyabiashara mdogo wa majiko ya kupikia yanayotumia mkaa pamoja na bidhaa nyingine, ndani ya soko la muda la Sabasaba, katika Halmashauri ya Mji wa Tarime, imebeba mengi.

Awali walifurahia biashara kuwa na sura ya neema kwao, lakini mabadiliko kutoka mipango ya serikali wilayani humo, kubomolewa jengo kupisha ujenzi mpya imezaa shida kwao. Kwa vipi? Fuatilia simulizi ya kilichowakuta wenyeji wake.



Mfanyabiashara mdogo wa majiko na bidhaa mbalimbali, Risu Joseph, akiwa kwenye biashara yake katika Soko la Muda la Sabasaba mjini Tarime. **PICHA ZOTE: ANTHONY GERVAS**

### MUUZA MAJIKO

Huyo ni Risu Joseph, mwenye simulizi ya namna maisha duni yanayomuelemea akiwa na familia yake ya watu wanane, akilalama umasikini unamuumiza maisha na akili yake, akiorodhesha kodi ya upangaji ‘inayomuendesha’ kumudu kulingana na uwezo wake kimaisha

Licha ya kodi ya vyumba hivyo vitatu, jumla yake Sh. 45,000 kwa maana ya kila chumba kinalipiwa Sh.15, 000 ambazo malipo yake yanatakiwa kila baada ya miezi mitatu. Risu anaendelea kufafanua:

“Naishi na familia nyumba ya kupanga isiyokuwa na sakafu wala umeme, yenye vyumba vitatu, natamani siku moja nipate pesa nijenga nyumba yangu ya kuishi ili niondokane na kero ya upangaji, kulipa kodi.”

Huku akitafsiri uhalisia wa maisha yake kuangukia umaskini, sasa anatamani walau siku moja kuwa mtu mwenye bashasha ya kufurahia maisha na familia yake, akihamia mazuri.

### KWANINI HAYO?

Swali ambalo Nipashe ilitaka kujua kulikoni hadi malalamiko hayo, mada kuu ikiwa janga la umaskini kwake? Hadi sasa analia na mzizi wa hali aliyonayo, ni kwamba soko kuu la zamani mjini humo kubomolewa miaka miwili iliyopita.

Ni hatua iliyochukuliwa na Halmashauri ya Mji Tarime, kupisha ujenzi wa soko jipya la kisasa, litakalokuwa kitega uchumi kikubwa cha mji, hata kuwaongezea pato la ndani.

> “Bado kiwango kinawazidi wenzao machinga, wanalipa kodi yakitambulisho cha Wajasiriamali Sh. 20,000 kwa mwaka.



Christina Emmanuel, akiuza bidhaa yake ya dagaa katika soko la Sabasaba, Tarime.

Anaeleza, tangu kubomolewa kwa soko mwaka 2019, ujenzi wake bado unasubiria bajeti, hali anayoitafsiri kwake imemuachia mtihani, akitamani ikamilike haraka na kuwawezesha wafanyabiashara wadogo warejee kwenye ulingo wao.

Kwa mujibu wa Risu, hadi sasa ni miaka 17, lakini bado haijamkomboa kwenye mtihani wa umasikini, akiendelea kutafuta mbadala wake wa kujinasua.

Risu anaeleza maisha binafsi, kwamba kero kuu inayomuelemea, ipo pale anapokosa pesa za kulipia pango la nyumba kwa wakati, hali inayomchanganya zaidi kwa madhila ya mwenye nyumba kumgongea mlango asubuhi kudai kodi, akimtaka mbadala wake ahame mara moja. Ni jambo mojawapo katika vilio vyake vya umasikini unaomjaza unyonge wa kutokuwa na uhakika wa maisha ya kila siku, mzizi ukianzia ugumu wa biashara katika soko la muda la Sabasaba.

Anasimulia kuna wakati hali hiyo ngumu inamlazimisha kufunga biashara hiyo na kwenda kutafuta kibarua mbadala, apate fedha za kulipa kodi ya nyumba.

“Biashara hii ya majiko naifanya kwa njia ya malikauli. Nachukua mzigo kwa mwenye duka, halafu naenda kuuza kwenye kibanda changu. Faida inayopatikana tunagawana, maisha yanaendelea kila siku. Sina mtaji wa kununua mzigo ‘keshi’ (taslimu),” anasema.

Anataja thamani ya jiko moja ananunua kwa Sh.1, 500, na kuuza Sh 2,000, huku akieleza ambayo ameizoea na kununua mzigo kwa pesa taslimu ili apate faida isiyokuwa na mgawanyo.

Mbali na ugumu wa soko, ambayo hadi sasa kila siku anauza wastani wa majiko mawili hadi manne na anataja wakati wa kiangazi, biashara yao inayumba zaidi kuliko wakati wa mvua, kwa sababu wateja wengi hutumia mbadala wa kuni.

### NAFUU YAO

Risu anataja upande mwingine wa nafuu, ni kwa Halmashauri ya Mji wa Tarime, kuwasaidia wafanyabiashara wadogo katika soko la muda kulipa kodi ya 20,000 kwa mwaka, tofauti na soko la zamani kulikobomolewa kupisha ujenzi walilipa Sh.50, 000 kwa mwezi.

Hata hivyo, anasema bado kiwango kinawazidi wenzao Machinga, wanalipa kodi ya Kitambulisho cha Wajasiliamali Sh. 20,000 kwa mwaka.

Anafurahishwa na mfumo mpya wa serikali katika ulipaji kodi kwa wafanyabiashara wadogo, kuwafutia utitiri wa kodi kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)

Pia anaieleza Halmashauri ya Mji Tarime, imewasaidia katika ulipaji kodi za sasa, ikiwa na unafuu kuliko zama zilizopita walipolazimishwa kulipa pesa zote mkupuo.

Rai yake ya sasa ni kwa Halmashauri ya Mji Tarime, kwamba ikamilishe ujenzi wa soko jipya la kisasa ili waweze kurejea uhalisia wa biashara zao wakiondoka kutoka soko hilo la muda, lililoko katika eneo analolitaja kuwa eneo la ‘maficho.’

### MUUZA DAGAA.

Mjasiriamali wa dagaa katika soko hilo, Christina Emmanuel, naye aliyeanza shughuli hiyo mwaka 2010, naye anaungana na Rissu, kwamba bado hali ni ngumu kibiashara, anakiri hali ngumu akiuza wastani wa kilomo mbili za dagaa kwea siku.

Mama huyu anasema kigumu kwake ni bidhaa zake zikapokaa muda mrefu pasipo wateja, anapata hasara ya kupungua uzito, huku binafsi hayo katika muugano wowote wa vikundi vya kinamama. Naye anakiri cha mtaji mdogo

### MKURUGENZI HALMASHAURI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mji wa Tarime, Elias Ntiruhungwa, anafafanua kuwa ujenzi wa soko kuu jipya la kisasa lenye ramani ya ghorofa moja,

“Serikali imeweka bajeti ya Sh. bilioni nne kwa ajili ya ujenzi wa soko hilo, ambalo bado hatujaanza kulijenga tunasubili fedha zikipatikana ujenzi unaanza mara moja mwaka huu, litakuwa na ghorofa moja,” anasimulia.

Mkurugenzi huyo anaeleza hana wasiwasi na hilo, kwamba atahakikisha anasimamia shughuli za maendeleo, ikiwamo miradi mbalimbali ya wananchi kufikia malengo ya halmashauri ya mji huo.


Anataja miradi mingi itatekelezwa kwa ufanisi, pamoja na ya kimkakati na isiyokuwa ya kimkakati, kwa ajili ya kukuza uchumi na kuongeza pato la mji wa Tarime.

Kauli hiyo ya Mkurugenzi Ntiruhungwa, inawapa matumaini makubwa wafanyabiashara wadogo wa Tarime na wananchi kwa ujumla wanasubiri neema pamoja na kutekeleza miradi mingine ya kiuchumi.

---

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Tushirikiane kujenga demokrasia, uchumi




KWA mara ya kwanza Aprili 22, mwaka huu, Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, alilihutubia Bunge la 12 la Tanzania, linaloendelea hivi sasa na mkutano wake Dodoma.

Rais alitoa mwelekeo wa serikali yake, akiainisha vipaumbele katika kuongoza nchi huku akirejea yale yaliyofanywa na mtangulizi wake, Rais Dk John Magufuli aliyefariki dunia Machi 17, mwaka huu.

Pamoja na kuahidi kuendeleza miradi ya kimkakati aliyoiacha Rais Magufuli na kubuni mingine mipya, kama kawaida yake, Rais Samia aliendelea na msimamo wake wa kutaka Watanzania kushikamana na kusahau mabaya yaliyopita.

Katika sehemu kubwa ya hotuba yake iliyokuwa mbashara, alihimiza maendeleo ya kiuchumi akisisitiza ushirikiano wa pamoja baina ya serikali yake na sekta binafsi, huku akitaka kodi iendelee kulipwa na kukusanywa kwa staha bila mabavu kama ilivyokuwa awali.

Rais Samia inaonekana anaamini kwa kiasi kikubwa, kwamba sekta binafsi hususan katika medani ya uwekezaji, ndiyo inaweza kuifikisha nchi katika maendeleo makubwa ya kiuchumi, hasa ikizingatiwa mtikisiko uliotokea baada ya baadhi ya watu kuondoa mitaji yao nchini.

Si siri kwamba, baadhi ya wafanyabiashara wamepitia kipindi kigumu sana cha uendeshaji biashara zao na hata kulazimika kufunga viwanda na kampuni na kuhamishia nchi zingine za kiafrika au Ulaya na Asia.

Hivi sasa, wapo wafanyabiashara wenye mitaji



**NA JOSEPH KULANGWA**
**(+255) 713 410008**
**jkulangwa@yahoo.com**

wanaodaiwa walikimbia nchi, ambao wanachungulia kuona kama mazingira yatawaruhusu kurudi kuendelea na uwekezaji.

Wapo walioko ndani wanaofikiria ‘kujifungua’ na kuanzisha biashara kubwa, lakini kwa kuangalia kwanza, kama kweli akisemacho Rais ndicho hasa ili wasije mbeleni wakajuta na kuishi kwa magumu kama ilivyotokea kwa baadhi.

Ni dhahiri, Rais Samia anapenda maridhiano, anapenda Watanzania waishi kwa haki na usawa bila kujali tofauti za kipato au itikadi na ndiyo sababu akaahidi kukutana na viongozi wa vyama vya siasa.

Anataka kufanya hivyo, ili kusikia changamoto zilizopo katika medani ya siasa, ndipo aone njia bora ya kufuata katika kujenga demokrasia, ambamo kila mtu atakuwa na fursa huru ya kuchangia mawazo yake na kuifanya nchi isonge mbele.

Katika hali isiyokuwa ya kawaida, Rais Samia alisikika akitoa mwito, kwa wabunge kuikosoa serikali yake, huku pia akiwataka kukataa wasiyoridhishwa nayo, ili mradi tu yanatoka kwa mawaziri wake.

Ni nadra sana kwa kiongozi wa nchi ambaye pia anakuwa kiongozi wa chama kinachotawala, kuruhusu wabunge wakiwamo wa upinzani, waikosoe serikali yake na wakatae ‘blahblah’ za mawaziri.

Inanikumbusha simulizi yake kabla hajawa mwanasiasa Zanzibar, alipokuwa akisikia mawaziri wakitoa majibu yasiyo sahihi kwa wawakilishi katika Baraza la Wawakilishi, kitu kilichompa hamasa ya kujiunga na siasa, hata akagombea ili akapambane na mawaziri wa aina hiyo.

Lakini ikawa bahati mbaya, hata alipochaguliwa, akajikuta anateuliwa kuwa Waziri na kibao kikamgeukia yeye, akawa ndiye wa kuzodolewa, lakini mchango wake ukatambuliwa mpaka kumsaidia kufika hapo alipo leo.

Hivyo Rais Samia anajua madhila ya watu kudanganywa kwa ‘blahblah’na ndiyo sababu akatoa ruhusa serikali yake kukosolewa ingawa kwa kujenga, lakini akiamini kwamba ni kwa njia hiyo tu, ndipo serikali kama ililala, itaamka na kuwahudumia wananchi.

Kitendo cha kukutana na viongozi wa kisiasa, ni hatua kubwa sana katika ujenzi wa demokrasia nchini. Bila shaka, viongozi hao wataitika mwito huo na kuhudhuria mkutano huo bila kususa, ambao ninaimani utakuwa mbashara, pia kwa wananchi, ili wafuatilie viongozi wao wanasema nini.

Asiishie hapo, baada ya hao akutane na makundi mengine, yakiwamo ya wanahabari, wafanyabiashara, wataalamu wa nyanja mbalimbali za kimaisha, walinzi wa amani na usalama na wengineo, ambao kwa namna moja au nyingine wana mchango katika nchi. Alamsiki!

UCHUMI

# Wizara Kilimo na JKT waingia ubia wa mapinduzi ya uzalishaji kitaifa

## • Katibu Mkuu, Meja Jenerali Mbuge wasaini • Mpunga kuzalishwa mara mbili kwa mwaka; kambi Chita kuwa kituo rasmi cha kimkakati



Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Gerald Kusaya (kushoto) na Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Meja Jenerali Charles Mbuge (aliyekaa kulia), wakitia saini mkataba wa kukuza mazao kwenye sekta ya kilimo nchini. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

**Na Renatha Msungu,** Dodoma

JESHI la Kujenga Taifa (JKT) na Wizara ya Kilimo, hivi karibuni wameingia mkataba wa ushirikiano katika kukuza sekta ya lilimo, ikiwamo kuzalisha mazao ya chakula na biashara kimkakati.

Katika mkataba huo wa miaka mitano, uliotiwa saini jijini Dodoma na Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo Gerald Kusaya na Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Meja Jenerali Charles Mbuge, maudhui ya makubaliano hayo yana sura endelevu, kwa kutoa nafasi ya kurudiwa, kila baada ya kufika mara kila inapofika ukingoni mwa muda tajwa.

Ni aina ya mkataba utakaotekelezwa kwa kufanya kazi pamoja, katika namna inayohakikisha sekta ya kilimo inasonga mbele na kunufaisha jamii kwa ujumla, mahsusi yakiangaliwa mazao ya biashara.

Hapo inaelezwa, ni namna ya kutimiza ndoto iliyokuwapo, Wizara ya Kilimo kutaka kufanya kazi pamoja na JKT, hasa ikizingatiwa umahiri iliyonayo katika kazi mbalimbali za maendeleo ambazo jeshi hilo inaendelea kuzitumikia.

Hadi sasa inaelezwa, JKT imejikita katika kilimo mkakati kwenye mazao ya chakula na kama vile mahindi, mpunga, maharagwe na mazao ya kibiashara inayojumuisha korosho, michikichi na kahawa.

> **"Mkataba wa ushirikiano kwenye sekta ya kilimo tulioanzisha, utasaidia sana kupiga hatua kwa hili tuliloanzisha kulifanya kwenye kilimo cha mkakati.**

### KATIBU MKUU KILIMO

Katibu Mkuu Kusaya, anatumia fursa hiyo kuipongeza JKT kutokana na kilimo mkakati wanachofanya, huku akisisitiza mkataba uliotiwa saini, ni kutimizwa ndoto ya muda mrefu ya kufanya kazi pamoja na JKT.

Anataja maeneo yatakayozingatiwa katika mkataba ni kuimarisha teknolojia bora za uzalishaji zinazoendana na wakati, kujenga uwezo katika usambazaji teknolojia za kilimo na kuboresha huduma za umwagiliaji.

Pia, anaorodhesha maeneo mengine yatakayozingatiwa kwamba ni utafutaji masoko na huduma za usimamizi wa mazao, ikiwamo suala la kuongeza thamani ya mazao yanayolimwa na JKT kama vile mpunga, mahindi na maharagwe, katika kambi zake mbalimbali.

Jingine analitaja ni kuwapo makubaliano yakatayoiwezesha Wizara ya Kilimo na JKT, kufanya tafiti za pamoja zitakazolenga mtazamo bora kwenye kilimo, kupitia uanzishwaji mpango mkakati wa pamoja, kusambaza taarifa za kilimo na teknolojia, huku wakibadilishana na taarifa za masoko zitakazopatikana katika mitandao.

"Tutafanya tathmini na usimamizi wa pamoja lengo ni kufahamu kile tulichokusudia katika makubaliano yetu kinakwenda sawa," anasema Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo.

Kwa mujibu wa Mtendaji Mkuu huo wa Wizara ya Kilimo, watakuwa wakifanya tafiti za pamoja kuhusu hali ya masoko na kisha wanalishauri jeshi, namna ya kukabili msimu husika wa kilimo, mazao ya kupandwa na kinachohitajika sokoni.

Eneo lingine analiloliainisha ndani ya msisitizo wake, ni mwendelezo wa ushirikiano walioanza na kinachofanya msaada ni kuiweka katika sura rasmi zaidi, hasa baada ya kuona jitihada zinazofanywa na JKT kukuza kilimo kitaifa.

### MKUU WA JKT

Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) Meja Jenerali Mbuge, anasema makubaliano hayo yaliyotiwa saini, yanahamasishwa pia na kuwapo nguvukazi ya vijana wengi wa kujitolea ndani ya JKT, ambako watapatiwa mafunzo ya stadi za kilimo yatakayowasaidia, hata baada ya kuhitimu na kurejea uraiani.

Meja Jenerali Mbuge anasema, jeshi ni sehemu muhimu ambayo ikitumika vyema katika ukuzaji kilimo, ni wazi italeta matokeo chanya, hasa kwa kukitumia vizuri kilimo katika ukuzaji uchumi wa nchi.

Kamanda huyo Mkuu wa JKT, anasema jeshi hilo katika mwaka wa fedha 2019/2020 na ilipo sasa, imeanzisha kilimo cha kimkakati katika kambi zake mbalimbali, huku katika kikosi cha Chita kilichoko wilayani Kilombero mkoani, Morogoro wana jukumu mahsusi la kuzalisha mpunga kimkakati kitaifa.

Meja Jenerali Mbuge anasema, zao hilo litakuwa linazalishwa mara mbili kwa mwaka kupitia skimu ya umwagiliaji na kwa sasa wanaendelea na ujenzi wa kikosi cha Chita JKT.

### KILIMO MKAKATI

Kaimu Mkuu Utawala wa JKT ambaye ni Mwenyekiti wa Kilimo Mkakati, Kanali Hassan Mabena, anasema wamechukua hatua za kuzalisha mazao ya chakula na biashara, ili kutimiza lengo la taifa kujitegemea kwa chakula, kupitia uzalishaji wa mazao hayo.

Anasema, katika kuimarisha uzalishaji, JKT imenunua zana za kilimo zitakazosaidia kuboresha sekta hiyo, huku Meja Jenerali Mbuge, akifafanua kwamba makubaliano hayo ni muhimu, hasa ikizingatiwa ni mkondo wa kijeshi ulio mstari wa mbele katika kutekeleza shughuli za kilimo.

Mwenyekiti wa Kilimo Mkakati wa JKT, Kanali Mabena, anafafanua kwamba wanachofanya sasa ni kuongeza ushirikiano wao katika namna yenye manufaa makubwa zaidi na wameshapanga kuifanya katika maeneo mbalimbali nchini.

Kanali Mabena, anataja vikwazo vinavyowakabili ni kuwapo upungufu wa wataalamu kilimo, mifugo na uvuvi ndani ya JKT, hivyo anaelekeza imani yake kwamba, ushirikiano walioanzisha sasa, utawaboresha na kuimarika zaidi kutekeleza shughuli za kilimo.

"Mkataba wa ushirikiano kwenye sekta ya kilimo tulioanzisha, utasaidia sana kupiga hatua kwa hili tuliloanzisha kulifanya kwenye kilimo cha mkakati," anasema Kanali Mabena.

Ombi lake kwa Wizara ya Kilimo, ni umuhimu wa kujengwa maabara kubwa ya kisasa kwa ajili ya kupima afya ya udongo, akiieleza ni jambo muhimu katika kumuwezesha mkulima kujua aina ya mazao anayopaswa kulima, kulingana udongo wa mahali aliko.

Kanali Mabena anasema, wakulima wengi kwa sasa hawana elimu ya afya ya udongo, ilhali ni mwongozo muhimu kwao katika kuwawezesha kutofautisha mazao ya kupanda katika msimu husika, kulingana na udongo uliopo sehemu husika, jambo linalosaidia kuvuna mengi.



# Waziri aiagiza NFRA kutafuta masoko mapya ya mahindi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, ameuagiza Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA), kutafuta masoko mapya ndani na nje kwa ajili ya kuuza shenena ya mahindi ya ziada yaliyopo kwenye maghala yao.

Prof. Mkenda aliyasema hayo juzi alipokuwa akizungumza na Menejimenti ya Wakala huo jijini hapa. Alisema hatua hiyo inalenga kulinda bei ya bidhaa hiyo isishuke na kuwakatisha tamaa wakulima.

Alisema kuwa suala la mahindi hivi sasa taarifa ni kuwa yanakwenda vizuri kutokana na wafanyabiashara kuanza kuuza bidhaa hiyo bila bugudha baada ya masoko kufunguliwa.

"Navishukuru sana vyombo vya ulinzi na usalama kwa kazi nzuri wanaoifanya hivi sasa, wafanyabiashara ya mazao ya mahindi wanafanya biashara hiyo bila kubugudhiwa," alisema.

Alisema amepokea taarifa ya usalama wa chakula inayoonesha Tanzania ina ziada ya tani 100,000 za mahindi na kuagiza NFRA kutafuta masoko haraka ili kunusuru uzalishaji wa zao hilo.

"Hivi sasa biashara ya mahindi kati ya Tanzania na Kenya inaendelea vizuri na hakuna yaliyokwama na Waziri wa Kilimo wa Kenya, Peter Munya, alikwenda Namanga kuangalia kama maelezo ya serikali yametekekezwa," alisema.

Alisema Tanzania haitegemei soko la upande mmoja na kuitaka sekta binafsi kuchangamkia masoko ya mazao nje ya nchi kwa kutafuta masoko ya mahindi na mchele.

"Nimepata taarifa wanaosafirisha mahindi hawapati bughudha tena kutoka kwa polisi, ushuru wa halmashauri lazima ulipwe, hatuwezi kuendeleza kilimo bila kuwa na masoko ya uhakika," alisema.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Bodi ya NFRA, Mhandisi Yustaki Kangole, alisema jukumu kubwa la wakala huyo ni kununua na kuhifadhi chakula na una uwezo wa kuhifadhi tani 250,000.

Alisema kwa sasa wana mradi wa ujenzi wa vihenge na ifikapo Juni, mwaka huu utakuwa umekamilika.



Baadhi ya waumini wa dini ya kiislamu wa madhehebu ya Answari Sunny, wakiswali swala ya Eid El Fitri katika Viwanja vya Mtekelezo, eneo la Mjini Mpya, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Waandishi watakiwa kuibua kero

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAANDISHI wa habari nchini wametakiwa kuibua kero zinazoikabili jamii na kutatuliwa kwa haraka na serikali.

Mkuu wa Wilaya ya Kongwa, Dk. Suleiman Serera, aliyasema hayo juzi katika maadhimisho ya uhuru wa vyombo vya habari Mkoa wa Dodoma yaliyoandaliwa na klabu ya Waandishi wa Habari Dodoma (CPC) kwa kushirikiana na muungano wa Klabu za Waandishi wa Habari Tanzania (UTPC), Mamlaka ya Hifadhi ya Taifa (TANAPA), pamoja na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira jijini hapa (DUWASA).

Akifungua maadhimisho hayo, kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Dkt. Binilith Mahenge, Mkuu huyo alisema vyombo vya habari vimekuwa na mchango mkubwa katika maendeleo ya taifa na kuwahimiza wanahabari kuendelea kuwa na ubunifu katika uchakataji wa habari.

Aliwaasa waandishi wa habari kuendana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia na kuhakikisha wanaandika habari zenye mizania ili kujiepusha kuleta migogoro kwa jamii.

Naye, Mwenyekiti wa CPC, Mussa Yusuph, alibainisha kero mbalimbali zinazoikabili tasnia ya habari kuwa ni pamoja na ubaguzi wa baadhi ya taasisi za serikali kutovialika baadhi ya vyombo vya habari kwenye matukio ya kitaifa.

Kwa upande wake, Ofisa Mhifadhi Mkuu wa TANAPA, Jully Lyimo, alisema sekta ya habari ina mchango mkubwa wa kukuza utalii nchini na kuwahamasisha waandishi wa habari kuandika fursa mbalimbali za utalii zilizopo nchini.

Katika maadhimisho hayo, tuzo mbalimbali zilitolewa kwa wadau ambao wamekuwa wakionesha ushirikiano mkubwa katika masuala ya habari.

Tuzo hiyo ilitolewa kwa Ofisa habari mwenye ushirikiano mzuri ambapo Innocent Lupenza kutoka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), alitunukiwa huku Sebastian Warioba, akipewa tuzo ya kuwa mwanachama bora wa CPC.

# 'Serikali haitavumilia mashirika yanayofanya kazi kinyume'

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, amesema serikali haitavumilia kuona mashirika yasiyo ya kiserikali yanafanya kazi bila kufuata sheria.

Dk. Gwajima alitoa kauli hiyo bungeni juzi katika hotuba ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Alisema serikali itaendelea kuimarisha ufuatiliaji na uratibu wa mashirika hayo ili yatoe mchango chanya wa ujenzi wa taifa na kunufaisha jamii.

"Pamoja na jitihada zinazoendelea kufuatilia na kuratibu shughuli za mashirika hayo, serikali itahakikisha jitihada zaidi inaongeza kukomesha mashirika yasiyotimiza masharti.

"Sitokubali kuona shirika lolote lisilo la kiserikali kuona linafanya kazi bila kusajiliwa kwa mujibu wa sheria sitovumilia hili litokee jisajilini mfanye kazi kwa utaratibu," alisema.

Alisema Sh. milioni 585.5 zimetengwa kwa ajili ya ufuatiliaji wa mashirika hayo 1,000 ya Tanzania bara.

"Pia kuna umuhimu wa kukuza uzalendo wa wananchi na ari ya kujitolea kujiletea maendeleo yao kwa kutumia rasilimali zinazowazunguka ambapo Sh. milioni 350.7 zimetengwa kufanikisha azma hii," alisema.

Kadhalika, alisema serikali itaendelea kuboresha mazingira ya kujifunza na kujifunzia na kuhakikisha wanawake wamepata nafasi zaidi za uongozi na uamuzi.

Kuhusu umuhimu wa makundi maalum katika jamii, Waziri Gwajima alisema, serikali itaendelea kuboresha huduma za ustawi wa jamii, kuboresha huduma kwa wazee, kufuatilia na kuimarisha uanzishaji wa vituo vya kulelea watoto wadogo na kuboresha huduma za usuluhishi wa migogoro ya ndoa na familia.

"Sh. bilioni 12.4 zimetengwa kwa ajili hiyo ikiwamo kukarabati majengo na miundombinu katika makazi 10 ya wazee ili kuwezesha kuwa na mazingira mazuri ya kulea wazee na wasiojiweza," alisema.

Alisisitiza kuwa wizara itaendelea kuratibu kampeni mbalimbali za kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto.

"Jumla ya Sh. milioni 791 zimetengwa kwa ajili ya kuratibu kampeni za kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto, pamoja na jitihada za serikali kukabiliana na vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto vitendo kama ukeketaji bado vinaendelea katika maeneo kadhaa nchini," alisema.





## Serikali kuendelea kuboresha miundombinu afya

**NA Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI mkoani Mbeya imesema inaendelea kufanya maboresho ya miundombinu ya afya katika maeneo mbalimbali ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora kwenye vituo hivyo.

Hayo yalisemwa juzi na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, wakati wa maadhimisho ya siku ya wauguzi kuwa kwa sasa serikali inaendelea kutoa elimu kwa wananchi kujenga zahanati kwenye vijiji na vituo vya afya kwenye kila kata.

Alisema mbali na maboresho ya miundombinu hiyo, pia ni sehemu ya uboreshaji wa mazingira ya kufanyia kazi kwa watumishi wa afya wakiwamo wauguzi.

"Kama mnavyofahamu katika hospitali yetu ya Kanda ya Rufani ya Mbeya hasa pale kitengo cha wazazi (Meta) tunaendelea na ujenzi wa jengo kubwa ambalo litakuwa na vyumba zaidi ya 200 ambalo litaondoa msongamano wa wagonjwa," alisema Chalamila.

Vilevile, alisema kuna ujenzi wa jengo la wazazi katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa ambalo litasaidia kuboresha mazingira ya wauguzi kufanya kazi na wagonjwa kupatiwa huduma kwenye mazingira rafiki. Alisema serikali inatambua mahitaji ya wauguzi na itaendelea kuwatekelezea kadri bajeti zitakavyokuwa zinaruhusu huku akiwataka viongozi wao kuendelea kuwaunganisha wauguzi.

Pia alisema kazi ya uuguzi ni ngumu na hivyo wauguzi wanatakiwa kutiwa moyo na viongozi wa serikali ili waendelee kufanya kazi hiyo ya kuokoa maisha ya watu kwa moyo.

Hata hivyo, aliwataka wauguzi hao kuepuka matumizi ya lugha mbaya kwa wagonjwa akidai kuwa lugha hizo huwa zinawakatisha tamaa wagonjwa na kuwafanya wananchi wakose imani na vituo vya serikali vya kutolea huduma.

# Washikiliwa tuhuma kuwaua wanawake kikatili

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, linawashikilia wanaume wawili mkoani humo kwa tuhuma za kuwaua wanawake kikatili kwenye matukio mawili tofauti likiwamo la mmoja kumuua mkewe kwa tuhuma za wivu wa mapenzi.

Akizungumza na waandishi wa habari katika Kituo Kikuu cha Polisi jana, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi, Ulrich Matei, alisema tukio la kwanza lilitokea katika Wilaya ya Kyela.

Alisema katika tukio hilo, Godlove Pimbi (50), mkazi wa Kijiji cha Lusonjo, Kata ya Matema, wilayani humo, anatuhumiwa kumuua mkewe, Elizabeth Mwaike (22), kwa kumpiga na kitu butu kichwani.

Alisema tukio hilo lilitokea Mei 11, mwaka huu, nyumbani kwa mtuhumiwa na chanzo cha tukio hilo kinadaiwa kuwa wivu wa mapenzi.

Ilidaiwa mtuhumiwa alikuwa anamtuhumu marehemu kuwa alikuwa na uhusiano na wanaume wengine. Kamanda Matei alisema mtuhumiwa baada ya kufanya tukio hilo aliubeba mwili wa marehemu na kwenda kuutelekeza umbali wa mita 500 kutoka nyumbani kwake kabla ya kudhibitiwa.

Alisema tukio la pili lilitokea Mei 11, mwaka huu katika mtaa wa DDC, Kata ya Utengule Usongwe, Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi, baada ya Chiku Abubakar (41), kushikiliwa kwa tuhuma za kumuua, Rose Mwandaje (45) kwa kumcharanga mapanga akishirikiana na wenzake ambao bado wanasakwa.

Kamanda Matei alisema mtuhumiwa pamoja na wenzake walimvamia Rose nyumbani kwake usiku saa 2:00 na kumkata mapanga maeneo mbalimbali ya mwili ikiwamo viganja vya mikono na nyuma ya shingo na kumsababishia kifo.

Alisema jeshi hilo linaendelea kuwasaka watuhumiwa wengine walioshiriki kwenye mauaji hayo ya kinyama ambao walitoroka baada ya tukio na kwamba watachukuliwa hatua kali za kisheria baada ya kukamatwa na kukamilisha upelelezi.

"Tunawataka wananchi waache tabia ya kujichukulia sheria mkononi wanapotofautiana, ni vyema wakamaliza tofauti zao kwa kufuata taratibu za kisheria, niwahakikishie wananchi kuwa tutawachukulia hatua kali wahusika wote," alisema Chalamila.

Katika hatua nyingine Kamanda Matei alisema, Mwasahala Nyunduru (32), mkazi wa Kabwe jijini Mbeya amefariki dunia baada ya kufukiwa na kifusi wakati akichimba mchanga katika eneo la Shewa, jijini hapa.

Alisema Nyunduru alifukiwa na kifusi Mei 11, majira ya jioni akiwa na wenzake wakichimba mchanga na kwamba chanzo cha tukio hilo ni mvua iliyokuwa inanyesha kulifanya eneo kuharibika.

Aliwataka wananchi wanaofanya kazi ya kuchimba mchanga kuwa makini kutokana na maeneo mengi kuwa hatari huku akiwataka wasitishe shughuli hizo.

Alisema mwili wa marehemu umehifadhiwa katika Hospitali ya Mkoa wa Mbeya wakati taratibu zingine zikiendelea kabla ya ndugu kukabidhiwa kwa ajili ya maziko.



Kijana mkulima akikokota baiskeli iliyosheheni mikungu ya ndizi, akielekea kuuza katika Soko la Ushirika, wilayani Rungwe, mkoani Mbeya, juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mgomo madereva daladala waingia siku ya tatu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MGOMO wa madereva wa daladala katika Jiji la Mbeya, umeendelea kutikisa kwa siku ya tatu na kusababisha wananchi wakiwamo wanafunzi kupata shida ya usafiri.

Madereva hao walianza mgomo huo Mei 11, mwaka huu, wakishinikiza serikali kutekeleza maazimio 10 ambayo walikubaliana yatekelezwe mwezi Machi likiwamo la kuziondoa pikipiki za magurudumu matatu kwenye barabara ambazo zimetengwa kwa ajili yao.

Kutokana na mgomo huo wananchi wanalazimika kutumia gharama kubwa za usafiri huku baadhi wakitembea kwa miguu umbali mrefu kwenda kwenye shughuli zao na baadhi ya wanafunzi wakishindwa kuhudhuria masomo.

Wakizungumza na Nipashe jana, baadhi ya wananchi walisema migomo hiyo ya mara kwa mara ya vyombo vya usafiri inakwamisha shughuli za uzalishaji mali na kuhatarisha uchumi wao kushuka.

Mmoja wa wananchi hao, Stephano Mwaiteleke, ambaye ni mfanyabiashara wa Soko la Sido jijini Mbeya, alisema katika kipindi cha miezi mitano kuanzia mwezi Januari mpaka sasa migomo ya vyombo vya usafiri katika mkoa huo imetokea mara nne.

Alisema ulianza wa mabasi yanayofanya safari zake kati ya Jiji la Mbeya na Kanda ya Ziwa ambao walikuwa na madai yao serikalini, ukafuata wa daladala, bajaji na kuibuka tena wa daladala.

Alisema migomo hiyo imekuwa ikisababisha wananchi kushindwa kufanya kazi zao kwa uhuru kwa sababu wanakuwa hawana uhakika wa kufika kwenye shughuli zao.

"Tunawaomba viongozi wetu wa mkoa kuingilia kati jambo hili ili migomo hii iishe, ni vyema wakayaita makundi haya yote na kujadiliana nayo namna ya kumaliza tatizo ili sasa watu tufanye shughuli zetu kwa amani," alisema Mwaiteleke.

Naye Maria John, alisema kwa sasa wazazi ambao watoto wao wanasoma mbali wanapata shida ya kutumia gharama kubwa kuwasafirisha kwenda na kurudi shuleni hali inayowafanya baadhi kushindwa kumudu.

Alisema yeye anakaa Mbalizi, lakini watoto wake wawili wanasoma Nzovwe, jijini Mbeya na kila siku analazimika kutumia zaidi ya Sh. 5,000 kuwahudumia ikiwamo nauli na chakula.

"Kila mtoto nalazimika kumpatia Sh. 3,000 kila siku ambazo 2,000 wanatumia kama nauli ya kwenda na kurudi na 1,000 ni kwa ajili ya chakula, sasa wanaenda wiki nzima na mmoja wa darasa la saba anaenda hata Jumamosi, natumia gharama kubwa sana," alisema Maria.

Hata hivyo, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Ulrich Matei, alisema jeshi hilo halina mpango wa kuziondoa bajaji hizo kama wanavyotaka madereva daladala.

Kamanda Matei alisema kwa sasa Jiji la Mbeya lina zaidi ya bajaji 3,000 ambazo zimeajiri vijana wengi na kuwa vigumu kuziondoa kwenye barabara ambazo madereva daladala wanataka.

Alisema ajira ambazo zimetolewa kwa vijana kutokana na uwapo wa bajaji ni miongoni mwa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) inayosisitiza vijana kujiajiri.



# Disco toto marufuku Eid el Fitri

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

KATIKA kusherehekea sikukuu ya Eid el Fitri, Jeshi la Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, limepiga marufuku kumbi zote za starehe kupiga mziki kwa ajili ya watoto (disko toto).

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa huo, Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP), Mohameed Salum Hamad, akitoa taarifa kwa vyombo vya habari,

alisema mmiliki yeyote atakayebainika kufanya hivyo atachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria ikiwamo kufikishwa mahakamani.

Alisema pia katika viwanja vya wazi vya kusherehekea sikukuu hiyo ni marufuku kupigwa mziki katika mkoa huo.

Aidha, alisema ni jambo la msingi kwa wamiliki wote wa kumbi hizo na viwanja vya sikukuu kuheshimu maelekezo yaliyotolewa na serikali ukiwamo muda wa kufunga viwanja na kumbi wakati wa sherehe hizo.

Alisema jeshi hilo limejipanga kuimarisha ulinzi ili kuhakikisha linadhibiti na kupambana na matukio yote yakiwamo ya uhalifu. Mohammed alisema jeshi hilo halitakuwa tayari kuwapa nafasi wahalifu wanaotumia sikukuu hiyo kufanya matukio ya kihalifu ikiwamo udhalilishaji kwa watoto.

Alibainisha kuwa jeshi litahakikisha linaimarisha ulinzi katika viwanja vyote vinavyosherehekewa sikukuu pamoja na kufanya doria katika fukwe za bahari na maeneo yote ya Mkoa kuhakikisha wananchi wanasherehekea katika hali ya amani na utulivu.

Kaimu Kamanda huyo aliwataka wazazi na walezi kuacha kuwavisha vitu vya thamani watoto wao ikiwamo dhahabu, kutowaacha pekee yao kwenda kwenye viwanja bila ya uangalizi wa wazazi au walezi wao ili kuwalinda watoto dhidi ya matukio mabaya.

Akizungumzia kuhusu fukwe za bahari ambapo baadhi ya watu huzitumia hasa katika kipindi hiki cha sikukuu, alisema wananchi ni vyema kuhakikisha wanaondoka katika maeneo yote ya fukwe ifikapo saa 12:00 jioni kwa mujibu wa maelekezo ya serikali.

Pia aliwatahadharisha wananchi kutoacha nyumba zao bila ya kuwa na mlinzi au mwangalizi ili kuepusha matukio ya wizi.

"Si vyema katika nyumba mkatoka watu wote kwenda kusherehekea bila ya kuwa na mtu yeyote au mlinzi," alisema Kaimu Kamanda huyo.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora Zanzibar, Haroun Ali Suleiman, akisoma hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya ofisi hiyo kwa mwaka 2021/2022, katika Kikao cha Baraza la Wawakilishi Chukwani Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Sheria zilizopitwa na wakati kupitiwa

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

TUME ya Kurekebisha Sheria ipo katika mchakato wa kuzifanyia mapitio sheria zilizopitwa na wakati kwa lengo la kwenda na mabadiliko ya kijamii, kiuchumi kisiasa na utamaduni.

Lengo lingine la mchakato huo likitajwa ni kuondoa mivutano katika utekelezaji wake.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Katiba, Sheria, Utawala Bora na Utumishi wa Umma), Haroun Ali Suleiman, wakati akiwasilisha makadirio mapato na matumizi ya bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2021-2022 katika Baraza la Wawakilishi.

Alisema zipo sheria zimetungwa katika kipindi cha tawala mbalimbali zilizopita, ambazo zinahitaji marekebisho pamoja na kufanyiwa tafsiri ya sheria yake ambapo nyingine zimepitwa na wakati na kusababisha utata katika utekelezaji wake.

Alizitaja sheria zinazotarajiwa kufanyiwa marekebisho kwenda na mabadiliko na tafsiri sahihi ni ya pombe za kienyeji nambari 164 ya mwaka 1942 na sheria ya makosa ya uzururaji namba 21 ya mwaka 1962.

Aidha, aliitaja sheria nyingine inayohitaji kufanyiwa marekebisho ni namba 4 ya mwaka 2005 ya kuwalinda wari, wajane na mtoto wa mzazi wa upande mmoja.

"Mheshimiwa Spika, Tume ya Kurekebisha Sheria kwa mwaka wa fedha 2021/2022 imejipanga kuzifanyia mapitio baadhi ya sheria kwa ajili ya kwenda na mabadiliko ya wakati na kuondosha migogoro na utata wa tafsiri kwa jamii," alisema. Aidha, alisema serikali inaendelea na mikakati yake ya kuimarisha taasisi zinazosimamia utawala bora ikiwamo Mamlaka ya Kupambana na Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA) pamoja na Tume ya Maadili ya Viongozi ili kuweka nidhamu katika matumizi ya serikali na fedha za umma kwa watendaji na wafanyakazi wa taasisi za serikali.

Alisema serikali imezitaka taasisi hizo kufanya kazi kwa kufuata maadili na sheria na hakuna kiongozi wa serikali atakayeingilia utendaji wa taasisi hizo katika uwajibikaji.

Waziri huyo aliliomba Baraza la Wawakilishi kuidhinisha jumla ya Sh. 60,312,975,000 kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ambapo kati ya fedha hizo, Sh. 37,613,800,000 ni kwa kazi za kawaida na Sh. 22,681,175,000 kwa miradi ya maendeleo.

## Wawakilishi wataka kauli ya SMZ kuhusu Ibada ya Hijja Makka

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi wameitaka serikali kutoa tamko kuhusu hatima ya safari za ibada ya Hijja huko Makka, kutokana na serikali ya Sauda Arabia kutoa masharti kwa waumini watakaofanya safari hizo kuhakikisha wanapata chanjo ya corona.

Waliyasema hayo wakati wakichangia hotuba ya makadirio mapato na matumizi ya bajeti ya Ofisi ya Rais (Katiba, Utawala Bora na Utumishi wa Umma) kwa mwaka wa fedha 2012/2022.

Mwakilishi wa Jimbo la Mfenesini, Machano Othman Said, alisema hadi sasa waumini wenye nia ya kufanya safari ya Hijja Makka hawajajua mustakabali wake wakati muda wa kutekeleza ibada hiyo ukiwa unakaribia.

Alisema waumini wa dini ya Kiislamu wenye nia ya kufanya ibada hiyo wamekuwa na wasiwasi mkubwa juu ya mustakabali wa safari hizo, ambazo ni miongoni mwa nguzo tano za dini ya Kiislamu kwa wenye uwezo wa kufanya hivyo.

Alieleza kwa mujibu wa masharti yaliyotolewa na Sauda Arabia kwa waumini watakaofanya ibada ya Hijja Makka, wawe wamepata chanjo kwa ajili ya kujilinda na ugonjwa wa corona ambao ni tishio kwa afya za wananchi wengi.

"Mheshimiwa Spika, tunaiomba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itoe tamko kuhusu hatima ya safari za ibada ya Hijja Makka, ambapo kwa upande wa serikali ya Sauda Arabia imetoa masharti kwa waumini watakaotekeleza ibada hiyo kuhakikisha wanapata chanjo ya kujikinga na corona," alisema.

Naye Mwakilishi wa Jimbo la Shauri Moyo, Hamza Hassan Juma, aliitaka Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana kuhakikisha wanajipanga vizuri kwa safari za Hijja, na kuondoa kasoro zinazojitokeza mara kwa mara.

Juma alisema safari za ibada ya Hijja katika mabadiliko ya mfumo mpya huwa zinaandaliwa na vikundi mbalimbali vya taasisi za Kiislamu, lakini kumejitokeza na kuibuka kwa kasoro mbalimbali zenye kusababisha usumbufu kwa waumini wa dini ya Kiislamu.

Kwa upande wake Mwakilishi wa Jimbo la Chaani, Nadir Abdulatif, aliitaka serikali kuchukua tahadhari kubwa kuhusu mpango wa chanjo ya corona inayotolewa sasa katika baadhi ya mataifa mbalimbali ambayo ufanisi wake katika afya ya binadamu umekuwa katika mjadala mkubwa.

"Mheshimiwa Spika, mimi siungi mkono kuhusu usambazaji na utoaji wa chanjo ya corona kwa wananchi wetu, kwa sababu bado chanjo hiyo haijatoa matokeo mazuri kwa afya za binadamu," alisema.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

***Uza,***
***Chenye Thamani Kubwa***
***Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa***
***Tupigie 0782253676***

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**KICHANGANI INVESTIMENT LTD** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **TVS STAR** yenye namba za usajili **MC 967 CQR**. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi **DOM/DOM/RB/ 242956/2021**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**SAMORA LEVISSON MDACHI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA CARINA** yenye namba za usajili **T 977 AXQ.** Chassis **No.AT2116014160**, Engine **No.7AG8O99O2**. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi **DOM/DOM/RB/239873/2021**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

MALAIKA UTALII TOUR LTD anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya LANDROVER-DEFENDER yenye namba za usajili T 886 CTB chasisi namba SALLDKWR7DA440194 engine namba 130620075448DT224,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa KIL/MOS/233035/2021

## KUPOTEA KWA CHETI



**BASHIRU MOHAMED LYENGITE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S0596-0072** kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia **LIWALE DAY SEKONDARI** mwaka 2013. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **RB/7257/2017.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**NDUGU PHILEMON MASALU** KAJOMOLA AMEPOTEZA KADI YA PIKIPIKI YENYE USAJILI **NAMBA MC849AGM** ILIYOKUWA NA JINA LA KAMPUNI YA TANZANIA CHINA & TOURISM DEVELOPMENT LTD ENGINE NAMBA **1p52fmhfa000339** KWA YEYOTE ATAKAEONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI RB NAMBA: **MOR/MOR/RB/246012/2021.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MWANZA**

**WILAYA NYAMAGANA MWANZA**
**SHAURI LA MIRATHI NO. 04 YA 2021**

**1. GILBERT WILLIAM MAKABE……...MWOMBAJI**
**DHIDI YA**
**2. JOYCE AMBROCE MOYO…………MAREHEMU**

**KWA YEYOTE YULE.**
**POPOTE ALIPO**

**KUITWA SHAURINI.**

Mtajwa hapo juu amefungua maombi ya kuomba kuteuliwa kuwa msimamizi wa mirathi ya marehemu JOYCE AMBROCE MOYO Mahakama hii imepanga kusikiliza shauri hilo mnamo tarehe 14/06/2021, saa 2:30 Asubuhi. Hivyo endapo kama kuna pingamizi lolote lile juu ya shauri hilo, liwasilishwe mahakamani tarehe tajwa hapo juu kabla mwombaji hajateuliwa na mahakama hii kuwa msimamizi wa mirathi.

**Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na mhuri wa mahakama hii leo tarehe 03/05/2021.**

……………………………………………
**HAKIMU MKAZI**
**WILAYA YA NYAMAGANA**
**MWANZA**

**USAFIRISHAJI MZIGO**

## TANGAZO

Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **JUMAMOSI** tarehe **15/05/2021** kampuni ya **LAL TRADING CO.LTD** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **DAR ES SALAAM** kuelekea **TANGA** kupitia **BAGAMOYO.**

Gari hilo lenye namba za usajili na vipimo vyake
**T 297 DTR/T 848 DUL UREFU 20 UPANA 4.8 KIMO 4.7**

Gari hilo linatoka **DAR ES SALAAM** kuelekea **TANGA** kupitia **BAGAMOYO** .Gari litasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:20 asubuhi mpaka saa 12:00 jioni)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI**
**INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042,**
**DAR ES SALAAM. MOB:**
**+255 - 0782253676**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Israeli yaongeza mashambulizi Gaza

**Gaza,** PALESTINA

MASHAMBULIZI kati ya Israeli na Palestina, yameendelea usiku kucha kuamkia juzi, katika machafuko ambayo yamesababisha vifo vya watu 65, wakiwamo watoto 14.

Hali ilivyo kati ya zote mbili, wakati huu Israeli ikisema imewaua makamanda wakuu wa Hamas, baada ya kushambulia jengo moja katika ukanda wa Gaza.

Umoja wa Mataifa (UN), ulisema kuwa iwapo hali hii haitasitishwa, huenda Israeli na Palestina zikaingia kwenye vita kamili.

Rais wa Marekani, Joe Biden alisema amezungumza na waziri mkuu wa Israel, kuhusu kinachoendelea.

Mpaka sasa haifahamiki ni lini makabiliano hayo yataisha, wakati Israel ikisisitiza kuwa itaendelea kulishambulia kundi la Hamas.

Machafuko hayo yalianza wiki iliyopita baada ya Wapalestina kuanza maandamano kupinga kuondolewa kwa nguvu, kuondoka eneo wanalosema ni ardhi yao, Mashariki mwa mji wa Jerusalem.

**RFI**

# Saba washambuliwa DRC na ADF

**Ituri,** DRC

WATU saba wameuawa katika kijiji cha Ngaka wilayani Mambasa mkoani Ituri, Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Mkoa huo hivi sasa unaongozwa na jeshi, baada ya rais wa nchi hiyo kutangaza kuwa pamoja na ule wa Kivu Kaskazini, uko chini ya uongozi wa jeshi kutokana na kudorora kwa usalama.

Waasi wa Uganda wa ADF, wananyooshewa kidole kuhusika na mauaji hayo.

Ni mara ya kwanza Wilaya ya Mambasa, mkoani Ituri kushuhudia mfululizo wa mashambulizi ya waasi wanaoshukuwa kutoka kundi la ADF, mwaka huu, kulingana na Idriss Kukodila, mkuu kiongozi wa wilaya hiyo.

"Kulikuwa na shambulizi katika kijiji cha Ngaka, walichoma nyumba kadhaa na kuiba mbuzi na kuku na kila walicho pendezwa nacho ingawa jeshi linaendelea kuwasaka waliotekeleza shambulio hilo," alisema Idriss Kukodila.

Manusura na mashahidi walisema, waasi hao waliingia na kuzingira vijiji vya Ngaka, Masana, Matonge na Sambango.

Mbali na mauaji ya raia na makumi ya wakazi wa vijiji hivyo kutekwa nyara na kubebwa msituni, kumeshuhudiwa pia uporaji wa mali ya umma na nyumba kuchomwa moto.

"Tunachoka na mauaji, wanatuondoa katika nyumba, tumefanya kosa gani! Tumekosea nini! Tunataka usalama hatutaki vita, raia wa kigeni warejee nchini."

Mei 8, mwaka huu, raia wengine wawili waliuawa mjini Lukaya, wilayani Mambasa na muasi mmoja kuuawa ziliripoti duru za Jeshi la FARDC.

**RFI**

# Mwili wa Mugabe kuzikwa upya

**Harare,** ZIMBABWE

MKE wa rais wa zamani wa Zimbabwe, Grace Mugabe, ameagizwa kufika mbele ya mahakama ya kitamaduni kwa tuhuma za kufanya mazishi yasiyofaa ya hayati Rais Robert Mugabe.

Waraka kutoka kwa Chifu Zvimba, ambaye ni mkuu wa kitamaduni wa nyumbani kwa kina Mugabe, unamtaka Grace, kuufukua mwili wa hayati Rais Mugabe ili uzikwe tena kulingana na utamaduni wa watu wa Zvimba. Grace, anatuhumiwa kwa kuenenda kinyume na utamaduni wa jamii yao kwa kumzika mume wake katika boma la familia, badala ya kumzika sehemu iliyochaguliwa na jamaa zake na mama yake.

Pia ameagizwa kulipa faini ya ng'ombe na mbuzi kwa kukiuka utamaduni.

Mugabe alifariki mwaka 2019 katika hospitali moja nchini Singapore, akiwa na umri wa miaka 95.

Familia yake iliamua afanyiwe mazishi ya faragha kijijini kwao Kutama, Wilaya ya Zvimba, karibu kilomita 90 sawa na maili 55, Magharibi mwa mji mkuu wa Harare, baada ya mvutano wa wiki kadhaa na serikali.

Patrick Zhuwao, mpwa wa marehemu rais, Alhamisi aliiambia televisheni ya Shirika la Utangazaji la Afrika Kusini, kwamba Mugabe alizikwa kulingana na ombi lake, uamuzi ambao unastahili kuheshimiwa.

Alisema hakuna mzozo ndani ya familia, akiongeza kwamba suala hilo lipo nje ya mamlaka ya chifu.

**BBC**



Mtoto akirushwa juu na baba yake, wakati baadhi ya watu walipokusanyika katika swala ya sikukuu ya Eid el-Fitri kwenye msikiti wa Al-Aqsa, uliopo mji wa zamani wa Jerusalem, Israel, jana. **PICHA: AP**

# Denmark kutoa hifadhi ya ukimbizi kupitia Rwanda

DENMARK imesema wageni nchini ambao wanataka kuomba hifadhi ya ukimbizi hivi sasa, watalazimika kufanya hivyo kupitia Rwanda, barani Afrika.

Ni jambo ambalo ni vigumu kuamini, ingawa huo ndio uamuzi uliofikiwa na mamlaka nchini Denmark.

Mfumo huo unaitwa usafirishaji wa ombi la hifadhi.

Hii ina maana mkimbizi, mhamiaji haramu, ambaye baada ya kuvuka bahari ya Mediterranean, anajikuta nchini Denmark na anaomba hifadhi nchini humo.

Pia atasajiliwa, kisha atawekwa kwenye ndege kwenda Rwanda, ambapo anaweza kuwasilisha ombi lake akiwa katika kituo cha wakimbizi. Mamlaka nchini Denmark, imekuwa inatafuta makubaliano na nchi kadhaa, ikiwa ni pamoja na Tunisia, Ethiopia, ingawa nchi hiyo na serikali ya Rwanda zimetia saini kwenye itifaki ya makubaliano.

Mazungumzo haya yote yalifanyika kwa miezi kadhaa na yalibaki kuwa siri, isipokuwa kwamba ofisa mmoja wa Rwanda, alivujisha siri hiyo baada ya kurusha kwenye Twitter picha yake akiwa na marafiki zake wapya kutoka Denmark.

Wengi walijiuliza maswali, lengo ni kupunguza uhamiaji haramu au la.

Waziri wa Uhamiaji wa Denmark, Mattias Tesfaye, ambaye ni mtoto wa mkimbizi, alisema atahakikisha kwamba mfumo huo utakuwa wa kibinadamu na wa haki zaidi.

Lengo ni kumfikia mhamiaji mmoja anasikika nchini Denmark.

**RFI**

# Waziri Mkuu Ivory Coast alazwa Paris

**Paris,** UFARANSA

WAZIRI Mkuu wa Ivory Coast, Patrick Achi, amelazwa katika hospitali ya Paris, Ufaransa, akiwa katika hali ya uchovu uliokithiri, kulingana na wasaidizi wake.

Patrick Achi, ambaye ni mpambe wa karibu wa Rais Alassane Ouattara, aliteuliwa kuwa waziri mkuu, Machi mwaka huu, kufuatia kifo cha mtangulizi wake, Hamed Bakayoko.

Patrick Achi mwenye umri wa miaka 65, atafanya vipimo vya kawaida katika hospitali hiyo jijini Paris na atapumzika katika nchini humo.

Kabla ya kurudi nchini mwake, vyanzo viwili vilinukuliwa na Shirika la Habari la REUTERS vilisema kuhusu taarifa hiyo.

Ivory Coast, ilipoteza mawaziri wakuu wawili waliokuwa mamlakani katika kipindi cha miezi kadhaa.

Amadou Gon Coulibaly, alifariki dunia kufuatia maradhi ya moyo mwezi Julai mwaka jana na Hamed Bakayoko, mwezi Machi mwaka huu, kwa maradhi ya saratani.

**RFI**

## HABARI MICHEZO




# INTER KUWAUZA LUKAKU, LAUTARO

**MILAN, Italia**

INTER Milan inaweza kulazimika kuwauza wachezaji wake nyota, Romelu Lukaku na Lautaro Martinez, kwa mujibu wa Corriere dello Sport.

Mastaa hao kwa pamoja wameisaidia Inter kushinda taji la Ligi Kuu Italia, Serie A, ikiwa ni kwa mara ya kwanza tangu msimu wa 2009-10.

Na sasa nyota hao wanaweza kulazimika kuuzwa kutoka hapo kwenye dimba la San Siro wakati Inter wakitaka kupunguza gharama.

Licha ya Kocha, Antonio Conte kuiwezesha Inter kupata taji hilo, lakini klabu hiyo inapitia kwenye matatizo makubwa ya kifedha baada ya mlipuko wa virusi vya corona.

Lukaku amekuwa akihusishwa na timu yake ya zamani Chelsea, Barcelona na Real Madrid, huku mchezaji mwenzake, Martinez kwa muda mrefu akihusishwa na Barca.

Alessandro Bastoni pia yupo kwenye orodha ya wanaohuishwa kuuza yeye akitajwa kuwaniwa na Manchester City pamoja na Liverpool, huku mlinzi wa pembeni, Achraf Hakimi amekuwa akihusishwa na Arsenal na Bayern Munich.

# TUCHEL

## AKUBALI KUBEBA LAWAMA KUFUATIA KICHAPO



**LONDON, England**

THOMAS Tuchel amesema yeye ndio wa kulaumiwa baada ya Chelsea kupokea kichapo cha bao 1-0 kutoka kwa Arsenal katika mchezo wa Ligi Kuu England pale katika dimba la Stamford Bridge, juzi Jumatano.

Pasi aliyoitoa Jorginho kurudisha mpira nyuma aliiwahi Emile Smith Rowe na kufunga bao hilo pekee dakika ya 16.

Chelsea walikaribia kufunga mara mbili kupitia Kurt Zouma na Olivier Giroud wote wakigonga mwamba.

Lakini Tuchel alitetea uamuzi wake wa kufanya mabadiliko saba kutoka kwenye kikosi kilichoifunga Manchester City 2-1 Jumamosi iliyopita.

"Kwa uhakika kabisa ni makosa yangu, na si mwingine yoyote. Nafikiri tumepoteza mchezo, lawama zote ni zangu," alisema akiiambia Sky Sports.

"Tulifanya mabadiliko makubwa. Tulifanya makosa mengi na tukawapa zawadi Arsenal kwa bao lao.

"Kwa ujumla hatukuwa kwenye kiwango cha kutosha cha kupata matokeo kwenye mchezo huu."

Chelsea sasa itacheza na Leicester City kwenye fainali ya Kombe la FA Jumamosi kabla ya kucheza fainali ya Ligi ya Mabingwa ifikapo Mei 29, mwaka huu.

# SIMEONE: ILIKUWA LAZIMA TUSHINDE

**MADRID, Hispania**

DIEGO Simeone amesema alijua Atletico Madrid walitakiwa kushinda baada ya vinara hao wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, na kukaribia kutwaa ubingwa baada ya kuwafunga Real Sociedad, Jumatano.

Baada ya Barcelona kupoteza pointi, Atletico walitakiwa kushinda mchezo wao ili kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kushinda taji la pili a ligi chini ya utawala wa Simeone na wakafanya hivyo kwa kupata ushindi wa 2-1 dhidi ya Sociedad.

Yannick Carrasco na Angel Correa kila mmoja alifunga bao moja ndani ya dakika 12 kuwawezesha Atletico kwenda mapumziko wakiongoza kwa 2-0.

Carrasco amehusika katika mabao 14 kwenye LaLiga msimu huu (mabao sita na pasi za mwisho nne).

"Tulijua kwamba tunatakiwa kushinda," alisema kocha wa Atletico, Simeone akiwaambia waandishi wa habari.

"Tulikuwa tukicheza na timu nzuri ambayo imekuwa ikifanya vizuri zaidi kwenye mechi za ugenini."



# JORGINHO

## KUPISHANA NA PJANIC BARCA

**BARCELONA, Hispania**

BARCELONA imeripotiwa kwamba inawaniwa kumsajili kiungo wa Chelsea, Jorginho kwa mabadilishano na kiungo wao, Miralem Pjanic endapo Blues hao watahitaji huduma ya mchezaji huyo.

Jorginho amekuwa na kipindi kizuri ndani ya Chelsea, lakini kocha wa timu hiyo, Thomas Tuchel ana mipango mikubwa msimu ujao ikiwamo kumsajili Pjanic ili kuongeza nguvu kwenye safu yake ya ushambuliaji.

Barcelona wanategemea kuendelea kubaki na Pjanic kutokana na uwezekano wa Georginio Wijnaldum kutoondoka kule Liverpool mwishoni wa msimu huu.

Na kigezo pekee cha kumwachia mchezaji huyo ni kubadilishana na Jorginho, ambaye amekuwa akifanya vyema sana tangu ujio wa Tuchel pale darajani.

Tuchel amekuwa mpenzi mkubwa wa Pjanic tangu alivyokuwa PSG na anaamini anaweza kuwa ingizo bora na muhimu sana kwenye timu ya Chelsea.

Pjanic hajawa na msimu mzuri sana pale Camp Nou msimu huu, huku akiwa amecheza michezo 28 na hajafanikiwa kufunga goli wala kutoa pasi ya bao.

Pia, hajacheza mchezo wowote wa LaLiga tangu Februari, mwaka huu.

## MOURINHO AMTAKA WHITE

**ROME, Italia**

KOCHA mpya wa AS Roma, Jose Mourinho anatajwa kumwania mlinzi wa Brighton, Ben White kama chaguo lake la kwanza la usajili katika kutengeneza timu itakayopigania taji la Serie A msimu ujao.

White amekuwa miongoni mwa walinzi bora msimu huu kwenye Ligi Kuu England akiwa na Brighton.

Endapo Roma watafanikiwa kuipata saini ya White, kuna uwezekano mabeki Gianluca Mancini na Marash Kumbulla wakawa kwenye nafasi ya kupata namba kwenye kikosi cha kwanza.

Mourinho alifukuzwa Tottenham kutokana na mwenendo mbaya wa timu hiyo kabla ya wiki iliyopita kutajwa kuchukua mikoba pale Roma.

Kwa sasa Mourinho amekuwa katika harakati za kuangalia orodha ya wachezaji ambao anaweza kutua nao Roma kwa ajili ya msimu ujao.

# BUFFON AKACHA KUTUA FLAMENGO

**TURIN, Italia**



GOLIKIPA wa Juventus, Gianluigi Buffon anasikilizia ofa mpya, lakini amekataa kujiunga na Flamengo wakati akionyesha hana mpango wa kustaafu.

Buffon ataondoka Juventus mwishoni mwa msimu huu, akiwa alijiunga tena na miamba hao wa Serie A miaka miwili iliyopita baada ya kuondoka msimu wa 2018-19 na kwenda Paris Saint-Germain.

Kipa huyo mwenye umri wa miaka 43 amekuwa akihusishwa na miamba wa LaLiga, Barcelona pamoja na klabu za Ligi Kuu Marekani (MLS), na Mashariki ya mbali, huku pia Flamengo wakiripotiwa kumwania.

Buffon alizungumzia kuhusu majaliwa yake baada ya kuokoa panalti kwenye mchezo wa Jumatano wa ushindi wa 3-1 dhidi ya Sassuolo.

"Nimepokea ofa kadhaa za kuvutia, nataka kuona ndani ya siku 20 kama zitakuja za kuvutia zaidi," alisema Buffon akiiambia Sky Sport Italia baada ya mchezo huo.

"Kama bado nataka kujihisi ni Buffon, nitapokea ofa. Vinginevyo nitastaafu."

Kuhusu ofa ya Flamengo, Buffon aliiambia TNT Sports Brazil: "Flamengo wamewasiliana na mimi ili kujiunga nao kama mchezaji huru, lakini nafikiri sitaikubali.

"Nitakaa jirani na Turin... hayo ndio matumaini yangu."

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# NEYMAR: NAHITAJI KUCHEZA NA RONALDO

Asema anataka kuona ushirikiano wao utakavyokuwa baada ya kucheza na mpinzani wake...

**PARIS, Ufaransa**

NYOTA wa Paris Saint-Germain, Neymar amesema anataka kucheza pamoja na Cristiano Ronaldo huku uvumi ukitawala juu ya majaliwa ya mkali huyo wa Juventus.

Ronaldo, ambaye amefikisha mabao 100 kwa Juventus baada ya mchezo wa ushindi wa Jumatano wa 3-1 dhidi ya Sassuolo, amedokeza anaweza kuondoka kwa miamba hao wanaosuasua kwenye Serie A mwishoni mwa msimu huu.

Mshindi huyo mara tano wa Ballon d'Or amekuwa akihusishwa na Paris Saint-Germain, na klabu za Manchester United na Real Madrid.

Na sasa nyota wa PSG, Neymar - ambaye amesaini mkataba mpya na mabingwa hao watetezi wa Ligue 1 amezungumzia kutaka 'upatina' na Ronaldo, akiwa tayari alishacheza na mpinzani wake, Lionel Messi kule Barcelona.

"Nataka kucheza na Cristiano Ronaldo," alisema mchezaji wa kimataifa wa Brazil mwenye umri wa miaka 29 akiiambia GQ.

"Tayari nimecheza na wachezaji wakubwa kama (Lionel) Messi na (Kylian]) Mbappe, lakini bado sijacheza na Cristiano Ronaldo."

Neymar mkataba wake wa sasa na PSG unamalizika mwaka 2025 baada ya kusaini mapema wiki hii.

Fowadi huyo alijiunga na mabingwa hao wa Ligue 1 akitokea Barcelona kwa mkataba wa miaka mitano kwa ada iliyoweka rekodi ya dunia ya euro milioni 222, Agosti mwaka 2017.

Mkataba mpya wa Neymar umeripotiwa kumfanya aingize kitita cha euro milioni 30 kwa msimu hapo Paris, ambako amefunga mabao nane kwa msimu huu katika mechi 16 kwenye mashindano yote.

## KWA UFUPI

**LAMPARD KUMRITHI HODGSON**

KOCHA wa zamani wa Chelsea, Frank Lampard ndiye anayeonekana kuwa mtu sahihi wa kuchukua nafasi ya Roy Hodgson katika klabu ya Crystal Palace. Mkataba wa Hodgson ambaye pia ni kocha wa zamani wa England unamalizika mwisho wa msimu huu. ***(Telegraph)***

**DORTMUND: HAALAND HAONDOKI**

OFISA Mtendaji Mkuu wa Borussia Dortmund, Hans-Joachim Watzke amesema mshambuliaji wao raia wa Norway, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 20, atabaki katika klabu hiyo msimu ujao. ***(ESPN, via Bild)***

**BARCA WAMTAKA FLICK**

BARCELONA wamewasiliana na wawakilishi wa kocha wa Bayern Munich, Hansi Flick, huu kukiwa na mashaka juu ya mustakabali wa hatima ya kocha wa sasa, Ronald Koeman katika klabu hiyo. ***(ESPN)***

**BUFFON ANUKIA BARCA**

BARCELONA wamefanya mawasiliano na golikipa wa Juventus, Gianluigi Buffon, ambae ataachana na kibibi kizee hicho cha Turin, mwishoni mwa msimu ***(Foot Mercato)***

**BAYERN YAMTOSA HAALAND**

OFISA Mtendaji Mkuu wa Bayern Munich, Oliver Kahn ametaja hatua yoyote ya uhamisho wa Erling Haaland ni "isiyofikirika" kwa sababu ya ada ya zaidi ya euro millioni 100 ambayo inazungumziwa. ***(Goal, via Bild)***

**SANCHO AAMUA KUFUNGUKA**

WINGA wa Borussia Dortmund na England, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 21, anamshinikiza wakala wake kufanikisha uhamisho wake wa kwenda Manchester United, baada uhaimisho huo kugonga mwamba msimu uliopita. ***(Manchester Evening News)***

**ROMERO AKARIBIA UNITED**

MANCHESTER United wanavutiwa na mlinzi wa Atalanta, Cristian Romero mwenye umri wa miaka 23 raia wa Argentina. ***(Sky Sports)***

**HOWE RASMI CELTIC**

KOCHA wa zamani wa Bournemouth, Eddie Howe, amekubali kuchukua mikoba ya kuifundisha klabu ya Celtic. ***(TalkSport)***

**SPURS YAMKODOLEA RODGERS**

KLABU ya Tottenham Hotspur wanajiandaa kuanza kumtafuta kocha mpya katika kipindi cha siku chache zijazo. Scott Parker wa Fulham ameorodheshwa, lakini klabu hiyo haijakata tamaa ya kumpata kocha wa Leicester City, Brendan Rodgers. ***(Football Insider)***

**SIMA AITAMANI EPL**

MSHAMBULIAJI wa Slavia Prague mwenye umri wa miaka 19 raia wa Senegal, Abdallah Sima, ambaye ananyatiwa na Arsenal na West Ham, anataka kuhamia Ligi Kuu England, EPL. ***(Standard)***

**CAMAVINGA AGEUKA LULU**

KIUNGO wa kati wa Rennes, Eduardo Camavinga mwenye umri wa miaka 18, "anasakwa na klabu kadhaa kubwa" kwa mujibu wa wakala wake, Jonathan Barnett, ambaye pia anamwakilisha Gareth Bale. ***(Goal)***

## HABARI MICHEZO

# MURO AITAKIA SIMBA MAFANIKIO KIMATAIFA

**Na Adam Fungamwango**

MKUU wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, ameitakia kila la heri Simba katika mechi yao ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Kaizer Chiefs inayotarajiwa kuchezwa kesho kwenye Uwanja wa FNB jijini Johannesburg nchini Afrika Kusini.

Muro ambaye alikuwa Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Yanga aliliambia gazeti hili anaungana na wanamichezo wote wa Tanzania kuwaombea Simba wafanye vyema katika mechi yao dhidi ya Kaizer Chiefs kwa sababu ikifanya vizuri, basi sifa inakuwa ni kwa taifa zima na si klabu hiyo peke yake.

Kiongozi huyo alisema anafahamu Simba inapeperusha bendera ya nchi, hivyo mafanikio itakayopata ya kusonga mbele katika mashindano hayo ya kimataifa yatakuwa na faida kwa timu zote.

"Ikishinda Simba hawasemi sifa haziendi kwa Clatous Chama, wala Luis Miquissone, inatasemwa ni Simba ya Tanzania, hawasemi Simba ya Zambia wala ya Msumbiji," alisema Muro.

Hata hivyo, Muro alisema kwa kiasi kikubwa Simba inabebwa na wachezaji wa kigeni, lakini kama ikitokea wachezaji hao wasiwapo kwenye klabu hiyo na wachezaji wa Kitanzania ndiyo waibebe kimataifa, isingeweza kufika hapo ilipo.

Mkuu huyo alisema linapokuwa suala la kitaifa mashabiki wote wa Tanzania wanatakiwa wawe kitu kimoja, lakini anachokiona ni kwamba wanaposhinda wanawatania mashabiki wa Yanga, kitu ambacho kinawafanya wakati mwingine wasiwe na umoja.

"Tatizo ni kwamba baadhi ya mashabiki wa Simba wakishinda tu, basi maneno yote na kejeli wanatupiwa mashabiki wa Yanga, sasa hiki ndiyo kinasababisha baadhi yao washindwe kuisapoti na kuiombea ishindwe," alisema Muro.

Simba inatarajiwa kucheza mechi ya kwanza ya hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika kesho kuanzia saa 1:00 usiku kwa saa za Tanzania, ndani ya dimba la FNB na marudiano yatafanyika Mei 22, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Wekundu wa Msimbazi walifika hatua hiyo baada ya kumaliza wakiwa vinara katika Kundi A huku nafasi ya pili ikishikwa na vigogo wa Misri, Al Ahly.



Kocha Mkuu wa KMC FC, Habib Kondo (mwenye kofia), akitoa maelekezo kwa wachezaji wake wakati wakifanya mazoezi kwa ajili ya kuwakabili Azam FC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa kesho Jumamosi hapa jijini Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

# Ihefu yafunguka kitakachowabeba

**Na Saada Akida**

BAADA ya timu yake kutoka sare ya bao 1-1 na Polisi Tanzania hapo juzi, Kocha Mkuu wa Ihefu SC, Zuberi Katwila amesema mbinu pekee itakayowafanya wapate matokeo mazuri na kuendelea kujiimarisha katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ni kucheza kwa nidhamu.

Ihefu yenye maskani yake Mbarali jijini Mbeya, inahitaji kuvuna pointi zaidi ili kujiondoa katika hatari ya kushuka daraja.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katwila alisema wanatakiwa kuwaheshimu wapinzani wao wote watakapokuwa kwenye mechi za ugenini ili kusalia katika Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

Katwila alisema malengo yao makubwa ni kuendelea kucheza ligi hiyo, lakini wakiimarisha mipango ya kubakisha pointi tatu katika mechi yao moja ya nyumbani ambayo imebakia.

"Matarajio yangu hata mechi zijazo za ugenini tutatumia mbinu za kuwaheshimu wapinzani wetu ili kupata matokeo bora, hakuna mechi rahisi, kikubwa ni kuendelea kujituma," alisema Katwila.

Ihefu FC yenye pointi 31 sasa iko katika nafasi ya 12 na mechi yao ya nyumbani iliyobakia ni dhidi ya Dodoma Jiji FC huku ugenini watafuata Kagera Sugar, JKT Tanzania, KMC FC na Yanga.

## Polisi Tanzania yaitisha Coastal

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Polisi Tanzania, Malale Hamsini, ametamba kikosi chake kiko kamili kwenda kuchukua pointi tatu katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Coastal Union itakayochezwa keshokutwa Jumapili kwenye Uwanja wa CCM, Mkwakwani jijini Tanga.

Malale alisema kwa sasa kikosi chake kiko imara baada ya wachezaji waliokuwa majeruhi kupona na kuwa fiti kwa pambano katika mechi hizo za lala salama. Malale alisema ana matumaini ya kuondoka na matokeo chanya katika mchezo huo dhidi ya Coastal Union ambao watakuwa na faida ya uwanja wa nyumbani.

"Tumeshindwa kuvuna pointi tatu ila tumepata moja dhidi ya Ihefu FC, sasa tunajiandaa kwa kufanyia kazi mapungufu yetu na kujiweka imara kwa ajili ya kwenda kuvuna pointi tatu tutakapowavaa Coastal Union, nina imani tutafanikiwa," alisema Malale. Aliongeza ligi imekuwa na ushindani mkubwa, na wakati wote wanawaheshimu Coastal Union ambayo pia imeendelea kujiimarisha katika kila idara kwa malengo ya kutimiza ndoto za kumaliza msimu kwenye nafasi nne za juu.

## Uchaguzi mkuu TWFA wakaribia

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha Mpira wa Miguu cha Wanawake Tanzania (TWFA), kinatarajia kufanya uchaguzi wake mkuu ifikapo Juni 26, mwaka huu imeelezwa.

Kwa mujibu wa tangazo lililotolewa na Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi ya TWFA, George Mushumba, mchakato wa kutoa fomu mbalimbali za wagombea ulianza jana na utamalizika Mei 20, mwaka huu.

Mushumba alitaja nafasi zinazowania katika uchaguzi huo ni pamoja na Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Katibu Mkuu na Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) ambazo ada ya kuchukua fomu ni Sh. 200,000.

Alizitaja nafasi nyingine zitakazowaniwa katika uchaguzi huo ni pamoja na Katibu Msaidizi, Mweka Hazina na wajumbe wanne wa Kamati ya Utendaji ambao nao watalipia kiasi cha Sh. 100,000 kwa kila fomu.

Alisema uchaguzi huo unafanyika kwa mujibu wa katiba na viongozi wapya watakaochaguliwa watakaa madarakani kwa muda wa miaka minne. Mara ya mwisho TWFA ilifanya uchaguzi wake mkuu Julai 8, mwaka 2017 na Amina Karuma alichaguliwa kuwa Mwenyekiti, Rose Kissiwa (Makamu Mwenyekiti), Somoe Ng'itu (Katibu Mkuu), Teddy Mung'ong'o (Katibu Msaidizi), Zena Chande (Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa TFF) na Hilda Masanche alichaguliwa kuwa Mweka Hazina.

# Michezo

Ijumaa Mei 14, 2021
Nipashe



NEYMAR: NAHITAJI KUCHEZA NA RONALDO HABARI UK 22



Wachezaji wa Yanga, Gift Mauya (kushoto) na Ditram Nchimbi wakifanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa kuwakabili Namungo FC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara inayotarajiwa kuchezwa kesho Jumamosi kwenye Uwanja wa Majaliwa ulioko Ruangwa mkoani Lindi. **PICHA: MTANDAO**

## GOMES: TUKO TAYARI

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA Mkuu wa Simba, Didier Gomes, amesema kikosi chake kina 'nguvu ya kutosha' kuwakabili Kaizer Chiefs katika mechi ya kwanza ya hatua ya robo fainali ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa FNB jijini Johannesburg, Afrika Kusini.

Gomes aliliambia gazeti hili amekamilisha maandalizi kuelekea mchezo huo huku akiongeza kila mchezaji ana kiu ya kupata matokeo mazuri katika mechi hiyo na kujiweka kwenye mazingira rafiki ya kusonga mbele.

"Tuko tayari na tuna nguvu ya kupambana, tumefanya mazoezi na tumekamilisha programu kuelekea mechi hii ya robo fainali, tunataka kuanza vyema hatua hii ili kujiweka salama katika mchezo wa marudiano tutakaocheza Dar es Salaam," alisema Gomes.

Nahodha na mshambuliaji wa timu hiyo, John Bocco amesema Simba ina kikosi bora na hali hiyo inawafanya wawe na imani ya kupata matokeo chanya dhidi ya Kaizer Chiefs.

"Wachezaji wote tuko vizuri, hatujawahi kukutana na Kaizer Chiefs, lakini tumepata nafasi ya kuwasoma, tunatarajia kuwa na mchezo mzuri na utakaotupa mwangaza wa wapi tunaelekea," Bocco alisema.

Aliongeza malengo ya Simba ni kuendelea kupeperusha vyema bendera ya Tanzania katika mashindano hayo yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), na hawataki kuonekana wamebahatisha kufika hatua hiyo.

# YANGA YAIPIGIA HESABU NAMUNGO

## Lengo ni kutimiza 'jambo lao' wakati Morocco ajipanga kuwavuruga vigogo hao na...

**Saada Akida na Adamu Fungamwango**

WAKATI Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi akisema kikosi chake kimeimarika zaidi kuelekea mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Namungo FC utakaochezwa kesho kwenye Uwanja wa Majaliwa, wenyeji wamedhamiria kubakisha pointi zote tatu nyumbani kwao.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nabi alisema wamejiandaa kukutana na ushindani katika mchezo huo, lakini kwao wanahitaji matokeo mazuri ili kujiimarisha kwenye mbio za kuwania taji la Ligi Kuu Tanzania Bara.

Nabi alisema watashuka dimbani kwa tahadhari kwa sababu wanafahamu wapinzani wao wameimarika kufuatia mechi za mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho walizocheza hivi karibuni.

"Tunakwenda kusaka matokeo bora na mazuri, tunajua matokeo hayo ndio yatatupeleka kwenye malengo yetu, nafasi ya ubingwa bado iko wazi na timu yangu inataka kuchukua kombe hilo msimu huu," alisema Nabi.

Naye Mkurugenzi wa Kamati ya Mashindano ya Yanga, Thabit Kandoro, alisema kurejea uwanjani kwa wachezaji wao tegemeo wakiwamo, Tuisila Kisinda na Saido Ntibazonkiza ni habari za faraja na zinazowaongezea nguvu.

Kandoro alisema hali katika kikosi chao ni nzuri na morali kwa kila mchezaji ni kubwa, hivyo wanaamini watafikia mikakati yao ya kuwachapa Namungo FC.

"Mazoezi yanaendelea vizuri, Nabi anaendelea kuwapa majukumu, kila mchezaji anaelekezwa atakachokifanya kuelekea mchezo huo ambao tunahitaji kurejea na pointi zote tatu muhimu za mchezo huo.

"Kisinda yuko fiti na kuna asilimia kubwa ya kupangwa katika kikosi kitakachoikabili Namungo FC, tunatambua wapinzani wetu wamekuwa wakitusumbua kila tunapokutana nao, iwe kwao au kwetu."

Malengo yetu bado yanaendelea kubaki vile vile kuhakikisha tunahitaji kutwaa ubingwa msimu huu, hatuwezi kufika huko hadi tushinde mechi zetu, Kocha Nabi ameshawapa majukumu wachezaji wake na sasa tunasubiri siku ya Jumamosi tukamilishe jambo letu," alisema Kandoro.

Aliongeza wanajiimarisha zaidi ili washinde mechi zao zilizobakia na kamwe hawatamwangalia mpinzani wao ambaye wanafukuzana katika mbio hizo za kuwania ubingwa.

"Mashabiki wanatakiwa kutulia kwani huu ni muda wa kupambana na kushinda mechi zetu, tusikubali kujipa presha na kuingia mitego ya mechi za wapinzani wetu ambao tunafukuzana katika kuwania taji," alisema Kandoro.

Naye Kocha Mkuu wa Namungo FC, Hemed Suleiman 'Morocco', amesema baada ya timu yake kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Mtibwa Sugar, hali ya kujiamini imerejea kwa wachezaji wake na sasa wako imara na tayari 'kuwapokea' Yanga.

Morocco alisema ushindi huo umekuwa ni 'dawa sahihi' kuelekea mechi hiyo dhidi ya Yanga ambao watacheza nyumbani na hawataki kuwaangusha mashabiki wao.

"Hatuko katika nafasi salama, ushindi umetuongezea nguvu katika mbio zetu za kujinasua, tumecheza mechi saa nane, hiyo ilitupa ugumu kidogo, lakini tulitawala mechi," alisema Morocco.

Aliongeza watashuka uwanjani kwa tahadhari kwa sababu wanafahamu Yanga imekwenda Lindi kusaka ushindi, hivyo hautakuwa mchezo rahisi kwa kila upande.

"Tunahitaji pointi kujiondoa mkiani, wenzetu wanahitaji ushindi ili kurejesha matumaini kwenye mbio za ubingwa, ni mechi ya kimkakati kwa kila timu, hatutarajii kuwaangusha mashabiki wetu na hasa tukiwa kwenye uwanja wa nyumbani," Morocco alisema.

Namungo FC yenye pointi 35 iko katika nafasi ya 10 kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara wakati Yanga yenye pointi 57 wako katika nafasi ya pili nyuma ya vinara na mabingwa watetezi, Simba walio na pointi 61 kibindoni.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002